

MIELEKEO YA JAMILUGHA YA KIMAASAI KUHUSU

KISWAHILI

KAINDI GLADYS NAISEI

C50/75693/2014

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KUTOSHELEZA BAADHI YA
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA
KISWAHILI YA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

2016

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu na wala haijawahi kutolewa popote kwa mahitaji ya shahada katika chuo kingine chochote.

Sahihi-----

Tarehe-----

KAINDI GLADYS NAISEI
(MTAHINIWA)

Tasnifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi na washauri tulioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi kupitia Idara ya Kiswahili.

Sahihi-----

Tarehe-----

DAKTARI NYACHAE MICHIRA
(MSIMAMIZI)

Sahihi-----

Tarehe-----

DAKTARI AYUB MUKHWANA
(MSIMAMIZI)

TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa mpenzi mume wangu Francis Kaesha ambaye ameonyesha upendo wa dhati na kuwa mhimili wangu kwa hali na mali.

Pia naitabarukia wazazi wangu wependwa marehemu babangu Daniel Kanoko na mamangu Josphine Njeri kwa kunilea na kunihimiza kusoma hadi kiwango cha juu. Kwa mama mkwe Grace Kamia mapenzi yake na maombi yalinitia moyo.

Hatimaye ni kwa wanangu wependwa Edwin, Grace na Duncan ambao uvumilivu wao mkubwa ulinipa sababu ya kujitolea kwa bidii niwe kielelezo kwao.

SHUKRANI

Shukrani zangu za dharti ninamtotea Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia uhai, mali, ujuzi na nguvu zilizoniwezesha kukamilisha kazi hii. Shukrani zingine ziwaendee mume wangu Francis Kaesha na wanangu Edwin, Grace na Duncan kwa kuwa wavumilivu na kwa kutokuwa na wao waliponihitaji. Aidha nawashukuru kaka zangu, dada zangu na mashemeji zangu wote kwa kuwa karibu nami na kunipa motisha ya kukamilisha yote yaliyohusiana na masomo yangu ya shahada ya uzamili. Mungu awabariki.

Shukrani jazila kwa wasimamizi wangu Dkt.Nyachae Michira na Dkt.Ayub Mkhwana waliojitotea kunielekeza kila nilipowahitaji na kufanikisha utafiti huu. Mwenyezi Mungu awe nanyi siku zote za maisha yenu.

Siwezi kusahau kuwashukuru wahadhiri wangu Prof. Abdulaziz, Prof. Mwenda Mbatia, Prof. John Habwe, Prof. Kithaka wa Mberia, Prof. Rayya Timmamy, Dkt. Zaja, Dkt. Mwaliwa, Dkt. Mbuthia, Dkt. Buregeya, Bi. Mary Ndungu, Dkt. Swaleh na Dkt. Mukhwana. Wataalamu hawa walinikuza kitaaluma hadi nikafikia kiwango hiki.

Ninamshukuru mwanadarasa mwenzangu Shadrack Kirimi tuliyeanza safari hii pamoja na mengi tuliofanya kwa ushirika tukihimizana hapa na pale tulipokumbana na changamoto kwenye safari ya usomi. Shukrani za dharti ziwaendee Wang'ang'a Njenga na Austin Anindo ambao walipiga taipu kazi zangu kwa uangalifu na subira kubwa. Siwezi kusahau kumshukuru Bw.Kanchaoi kwa msaada wake mkubwa aliyonipa na hivyo kuniwezesha kufanikisha kazi hii. Nawashukuru sana wengine wote ambao walinisaidia kwa njia moja au nyingine na ambao siwezi kuwataja, nasema asante sana Mungu awe nanyi daima.

IKISIRI

Katika tasnifu hii, tumechunguza mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu Kiswahili. Utafiti wenyewe umejikita katika kuchunguza masiala yanayosababisha lugha ya Kiswahili ambayo ni rasmi Kenya kutotumika katika diskosi rasmi katika tarafa ya Kitengela wilayani Isinya kaunti ya Kajiado. Mbinu tulizotumia ni hojaji za kujazwa na mahojiano ya moja kwa moja. Tuliweza kutumia maswali ya wazi, maswali funge na maswali ya viwango. Waliopendelea lugha yao ya asili katika kujaza hojaji walipewa maswali yaliyokuwa katika lugha ya Kimaasai. Viongozi mbalimbali pamoja na wakazi wa umri mkubwa na mdogo wenye asili ya Kimaasai ndio waliohusishwa katika mahojiano pamoja na kujaza hojaji. Data ilichanganuliwa kwa kutumia baa grafu, majedwali ya frikwenzi pamoja na pai chati. Nadharia jumuishi na utambulisho ya Giles (1979) ndio iliyotumika. Matokeo ya utafiti yalikuwa kwamba jamiilugha ya Kimaasai katika tarafa ya Kitengela ina mielekeo hasi na chanya kuhusu lugha ya Kiswahili kwa kutegemea viathiriwa vilivyotumiwa. Watafitiwa walio na umri mkubwa walithamini lugha ya Kimaasai ikiwa ni lugha ya jadi kwa madhumuni ya kudumisha utamaduni, imani, mila na desturi. Walio na umri mdogo wanaendelea kupoteza umilisi wao wa lugha asili kutokana na hali ya mabadiliko ya maisha ya jamii ya Wamaasai kadri miaka zinavyozidi kupita. Mapendekezo yalikuwa, kwa kuwa lugha ya Kiswahili ni rasmi viongozi watumie katika mikutano rasmi kwani ndio lugha inayoweza kuleta hisia za undugu na mshikamano miongoni mwa jamiilugha mbalimbali.

YALIYOMO

UNGAMO.....	i
TABARUKU	ii
SHUKRANI.....	iii
IKISIRI.....	iv
SURA YA KWANZA	1
1.0 Utangulizi.....	1
1.1. Tatizo la utafiti	3
1.2. Madhumuni ya utafiti.....	4
1.3. Nadharia tete	4
1.4. Sababu za kuchagua mada	5
1.5. Upeo na mipaka	6
1.6. Yaliyoandikwa kuhusu mada	7
1.7. Msingi wa kinadharia.....	11
1.8. Njia za utafiti.....	13
1.8.1. Ukusanyaji na uchanganuzi wa data	13
SURA YA PILI	16
2.0 Historia ya Maendeleo ya Kiswahili Kajiado	16
2.1 Utangulizi.....	16
2.2 Kiswahili Kajiado kabla ya Uhuru.....	18
2.3 Kiswahili Kajiado baada ya Uhuru	20
2.3.1 Kiswahili Kajiado enzi ya Kenyatta	23
2.3.2 Kiswahili Kajiado enzi ya Moi.....	27
2.3.3 Kiswahili Kajiado enzi ya Kibaki na Uhuru	31
2.4 Hitimisho.....	33
SURA YA TATU.....	35
3.0 Uchanganuzi wa Data	35
3.1 Utangulizi.....	35
3.2 Watafitiwa katika utafiti.....	35
3.2.1 Vipengee vilivyotafitiwa	38

3.2.2 Kipengee cha tofauti za kiumri na jinsia	38
3.2.3 Kipengee cha kazi aifanyayo mtu	40
3.2.4 Kipengee cha makazi	42
3.2.5. Kipengee cha kiwango cha elimu	43
3.2.6 Kipengee cha lugha inayotumiwa kanisani	45
3.2.7 Viongozi	46
3.3 Muhtasari wa vipengee vilivyotafitiwa.....	47
3.3.1. Uchanganuzi wa data ya walengwa.....	49
3.3.2 Tofauti za umri na jinsia.....	50
3.3.3 Kazi aifanyayo mtu	52
3.3.4 Makazi	53
3.3.5 Kiwango cha elimu.....	54
3.3.6 Lugha inayotumika Kanisani.....	54
3.3.7 Viongozi	55
3.3.8 Hitimisho	56
SURA YA NNE	57
4.0 Mjadala Kuhusu Mielekezo Dhidi ya Kiswahili Kitengela.....	57
4.1. Utangulizi.....	57
4.2. Tofauti za jinsia na umri	57
4.3. Kazi aifanyayo mtu	58
4.4. Makazi.....	59
4.5. Kiwango cha elimu	59
4.6. Lugha inayotumika kanisani	60
4.7. Viongozi.....	60
Hitimisho.....	61
SURA YA TANO	62
5.0 Muhtasari, Hitimisho na Mapendekezo.....	62
5.1 Utangulizi.....	62
5.2 Muhtasari	63
5.3. Hitimisho.....	64
5.4 Mapendekezo	66

MAREJELEO	68
VIAMBATANISHO	I
Kiambatisho cha kwanza	I
Kiambatisho cha pili	II
Kiambatisho cha tatu.....	VIII
Kiambatanisho cha nne	XII
Kiambatanisho cha tano	XVI
Kiambatanisho cha sita	XIX
Kiambatanisho cha saba.....	XXIV
Kiambatanisho cha nane	XXVIII
Kiambatanisho cha tisa	XXIX

SURA YA KWANZA

1.0 Utangulizi

Kiswahili ni lugha muhimu sana katika maisha ya kila siku ya Wakenya kwa kuwa ni lugha ya taifa na ndiyo lugha ambayo haiibui hisia za kikabila miongoni mwa wazungumzaji wake. Kwa mujibu wa KemboSure (1996), watu wengi nchini Kenya hujifunza lugha hii kwa sababu inaashiria umoja wa kitaifa. Kiswahili hutumiwa kama chombo cha mawasiliano baina ya watu wa makabila tofauti tofauti. Kiswahili ni miongoni mwa lugha za Kiafrika zilizofanyiwa utafiti mwingi sana (Mbaabu 1991).

Kuna ithibati zinazoeleza mengi, tangu chimbuko na historia ya lugha hii, maendeleo yake, jinsi ilivyosambaa, hadhi yake katika ngazi za kitaifa na za kimataifa pamoja na jukumu inayotekeleza kama lugha ya mawasiliano mapana (Mbaabu 1991; Chimera 1998). Lugha ya Kiswahili imeenea na inazungumzwa pahali pengi Afrika mashariki na kati, yaani Tanzania, Kenya, Uganda na katika baadhi ya sehemu za Rwanda, Burundi, Msumbiji, Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia, Malawi, Komoro na Afrika Kusini (Massamba na wenziwe 2001:02).

Nchini Kenya lugha ya Kiswahili hufundishwa kama somo la lazima katika shule za msingi na za upili. Hufundishwa pia vyaoni ambapo hutahiniwa kama somo la hiari. Kadhalika, Kiswahili hutumika kutangazia katika idhaa mbali mbali za redio nchini Kenya na isitoshe, idhaa za kimataifa kama vile Shirika la Utangazaji la Uingereza (B.B.C) Sauti ya Amerika (V.O.A) Shirika la Utangazaji la Ujerumani hutumia lugha ya Kiswahili katika matangazo

yao. Vilevile baadhi ya mashirika ya kuchapisha magazeti hutumia lugha ya Kiswahili katika baadhi ya matoleo yao, hususan *Taifa Leo* nchini Kenya.

Katika mawanda ya kijamii, biashara na hata kisiasa, idadi kubwa ya Wakenya huwasiliana kwa kutumia Kiswahili zaidi ya lugha nyingine yoyote (Moseti, 2002). Katika eneo pana la Afrika mashariki na kati Kiswahili ndiyo lugha sambazi inayoongoza kwa kuzipiku lugha zingine (Chimera, 1998;1). Jambo hili limewezekana licha ya kuwa eneo hili lina idadi kubwa ya lugha za kienyeji pamoja na kuwepo kwa upinzani wa lugha za kigeni kama vile Kiingereza na Kifaransa. Lugha ya Kiswahili imeenea na kukua kiasi cha kuweza kupambana na zingine katika ngazi za kimataifa, kimatumizi na kimajukumu.

Hata ingawa lugha ya Kiswahili ina umuhimu mwingi na majukumu mengi, bado inakumbana na pingamizi nyingi mno. Uchunguzi wa matumizi yake unaonyesha kuwa hali yake bado hairidhishi (Mohochi 2011). Miongoni mwa vikwazo hivyo ni mielekeo ya lugha inayobainika katika jamiilugha ya Wakenya (Mukhwana, 2008).

Utafiti huu umejikita katika mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu Kiswahili. Mielekeo ya watu kuhusu vitu au dhana fulani huweza kuwa na athari kwa kitu au watu hao husika. Kwa misingi hii kuna maana kuwa mielekeo ya watu kuhusu lugha huweza kuathiri namna watu huitazama lugha husika. Mielekeo kuhusu lugha hutokana na visababishi fulani. Kufuatana na haya ndipo ambapo tulitafiti mielekeo kuhusu Kiswahili miongoni mwa jamiilugha ya Kimaasai katika tarafa ya Kitengela wilayani Isinya kaunti ya Kajiado.

Wilaya ya Isinya katika kaunti ya Kajiado ina wazungumzaji wa kabila mbalimbali kutoka sehemu nyingi za nchi ya Kenya. Makabila hayo ni kama vile; wazungumzaji wa lugha za Kimaasai, Kikikuyu, Kikisii, Kikalenjini, Kibaluhya na Kijaluo. Kunao vilevile Wasomali na Wahindi wachache. Jamiilugha ya Kimaasai ndio iliyo kubwa zaidi ya yote ambapo imeenea kutoka Isinya hadi kwenye mpaka wa Kenya na Tanzania.

1.1. Tatizo la utafiti

Kupatikana kwa makabila mbalimbali katika tarafa ya Kitengela kunatazamiwa kwamba lugha ya mawasiliano iwe Kiswahili katika shughuli nyingi na miktadha mbalimbali. Kwa mujibu wa Iribemwangi na Mukhwana (2011), lugha ya Kiswahili hutumiwa kuwaleta pamoja wanajamii mbalimbali kimawasiliano. Hutumika vilevile kujenga, kuendeleza na hata kudumisha uchumi biashara na umoja miongoni mwa jamii mbalimbali. Licha ya hayo, lugha ya Kiswahili kama lingua franca huleta ushirikiano miongoni mwa watu walio na tamaduni mbalimbali kwa kuwaleta pamoja. Lugha ya Kiswahili aghalabu haitumiwi kama inavyotarajiwa katika diskosi rasmi katika tarafa ya Kitengela, hali ambayo imeibua hisia za umuhimu wa kufanya utafiti.

Utafiti huu uliangazia mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu Kiswahili ambapo tuliangazia yanayosababisha lugha hii ya taifa kutotumiwa mara kwa mara katika miktadha rasmi kama vile; katika mikutano ya viongozi wa kisiasa, baraza la chifu, makanisani na kwenye sherehe mbalimbali tarafani. Kwa kutumia viathiriwa kama vile tofauti za jinsia na umri, makazi, kazi aifanyayo mtu, viongozi, kiwango cha elimu na lugha inayotumika kanisani tuliweza kutambua visababishi vya mielekeo walio nayo jamiilugha ya Kimaasai kuhusu lugha ya Kiswahili.

Lugha ya Taifa ni lugha ambayo inatumiwa kama utambulisho wa taifa. Katika nafasi hiyo lugha husika inakuwa na hadhi ya juu na kuheshimiwa na serikali na wanajamii. Katika matumizi rasmi na yasiyo rasmi lugha hii inapaswa kupewa kipaumbele cha kwanza kwa kila hali ambapo wanajamii wanatarajiwa kuitumia kubuni na kueleza fikra na mitazamo yao ya ndani na vilevile kueleza hisia zao za ndani. Lugha hii pia ndiyo inayopaswa kutumiwa kupangia mambo yote ya maendeleo ya jamii (Msanjila na wenzake, 2009).

Kwa kuchunguza mielekeo ya washika dau kama vile viongozi wa jamiilugha ya Kimaasai kuhusu Kiswahili tutaweza kutathmini uhusika na ukubalifu wao na hivyo, ushawishi wao katika utekelezaji wa sera ya lugha nchini Kenya.

1.2. Madhumuni ya utafiti

- a) Kuchunguza mielekeo tofauti tofauti kuhusu lugha ya Kiswahili miongoni mwa jamiilugha ya Kimaasai inayoishi katika tarafa ya Kitengela wilayani Isinya kaunti ya Kajiado
- b) Kuchunguza sababu zinazochangia kuwepo kwa mielekeo kuhusu lugha ya Kiswahili katika tarafa ya Kitengela miongoni mwa viongozi mbalimbali na wakazi wa jamiilugha ya Kimaasai
- c) Kuchunguza iwapo mielekeo kuhusu lugha ya Kiswahili ina athari kwa lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa nchini Kenya miongoni mwa wakazi wa Kitengela

1.3. Nadharia tete

- (a) Jamiilugha ya Kimaasai inayoishi katika tarafa ya Kitengela wilayani Isinya kaunti ya Kajiado ina mielekeo tofauti tofauti kuhusu lugha ya Kiswahili .

- (b) Kuthamini lugha kwa jamiilugha ya Kimaasai kumepelekea kwa wao kuwa na mielekeo kuhusu lugha ya Kiswahili.
- (c) Mielekeo kuhusu lugha ya Kiswahili ina athari kwa lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa nchini Kenya miongoni mwa wakazi wa Kitengela.

1.4. Sababu za kuchagua mada

Kiswahili ni lugha ya taifa na lugha rasmi ambayo inapaswa kutumika katika mawasiliano rasmi na ya kitaifa nchini Kenya. Kutotumika kwa lugha hii kama inavyotarajiwa katika miktadha mbalimbali kama vile kwenye mahubiri kanisani, mikutano ya kina mama na wazee, baraza la chifu mikutano ya kisiasa na jamiilugha ya Kimaasai katika tarafa ya Kitengela kulinipa motisha ya kuangazia mielekeo ya jamiilugha hii kuhusu Kiswahili na visababishi vya mielekeo hiyo.

Vilevile tafiti nyingi zimefanywa kuhusu mielekeo ya wanajamii kuhusiana na lugha nchini Kenya. Hata hivyo tafiti hizi hazijashughulikia mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu Kiswahili katika tafa ya Kitengela. Uchunguzi wa mielekeo kuhusu lugha ya Kiswahili miongoni mwa jamiilugha ya Kimaasai kutatusaidia kutambua athari zake kwa lugha ya Kiswahili kama jinsi ilivyo lugha rasmi na ya Taifa.

Katika isimujamii, suala la upangaji lugha na sera lina umuhimu mkubwa. Ni katika muktadha huu ambapo suala la mielekeo linadhihirisha umuhimu wake (Edwards, 1985). Mielekeo huathiri hadhi inayopewa lugha nayo hadhi inaathiri matumizi na harakati za kuiendeleza lugha husika Holmes (1992). Wapanga sera za lugha nchini na katika sekta ya

elimu watafaidi kutokana na matokeo ya utafiti katika kuandaa sera zitakazolenga kuboresha hali ya lugha ya Kiswahili nchini Kenya. Aidha matokeo yatakuwa msingi wa kutoa mapendekezo ya kuimarisha lugha miongoni mwa wasomi.

Ripoti ya utafiti huu itakuwa mchango wa maandishi ya kitaaluma katika isimujamii kuhusu mielekeo ya lugha na hasa mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai. Walimu wanaofundisha somo la Kiswahili wataweza kujua jinsi ya kukumbana na visababishi vya mielekeo kuhusu lugha ya Kiswahili ambavyo huweza kuathiri ufundishaji wa somo la Kiswahili miongoni mwa watu wa jamiilugha ya Kimaasai katika Tarafa ya Kitengela. Utambuzi wa visababishi vya mielekeo kuhusu lugha ya Kiswahili utawezesha hatua mwafaka kuchukuliwa ili Kiswahili kiweze kupata fanaka inayostahili na pia kithaminiwe na jamiilugha ya Kimaasai inayoishi katika tarafa ya Kitengela.

Lugha ya Kiswahili pia itaweza kutekeleza majukumu yake kama inavyostahili. Kwa mujibu wa Buliba. A(2006), lugha ya taifa ina jukumu la kuwaunganisha watu kutoka makabila mbalimbali au maeneo mbalimbali katika taifa ili kuweza kushirikiana na kufanya kazi pamoja kwa manufaa ya taifa lao. Hivyo basi, kwa kutafiti mielekeo ya watu wa jamiilugha ya Kimaasai Kitengela, tutaweza kuioanisha mielekeo hii na ya Wakenya wote ili watu wa Kitengela wasiwachwe nje ya utangamano wa taifa zima la Wakenya.

1.5. Upeo na mipaka

Utafiti huu ulihusu mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu lugha ya Kiswahili. Ulijikita tu na eneo la tarafa ya Kitengela wilayani Isinya kaunti ya Kajiado. Viongozi mbalimbali

kama vile wa makanisa, wa kisiasa waliochaguliwa na walioteuliwa, machifu pamoja na manaibu wao, viongozi wa vijij na baadhi ya wakazi wa tarafa ya Kitengela ndio tuliowahusisha katika mahojiano na kujaza hojaji. Kwa kuwa wateuliwa hawa waliwakilisha miktadha mbalimbali, uhusika wao uliweza kutupa matokeo ya uchunguzi wetu.

Sababu za kuteua tarafa ya Kitengela ni kuwa ni eneo la wingilugha kutokana na uuzaji na ununuzi wa ardhi unaoendelea humo kwa wingi pia ni mji ambao hauko mbali sana na Nairobi ambao ni mji mkuu wa Kenya na lugha ya Kiswahili ambayo ndio lugha rasmi ilitarajiwa kutumiwa katika mikutano. Walioteuliwa kujaza hojaji na pia kwa mahojiano walikuwa wa jamiilugha ya Kimaasai na walituwezesha katika utafiti wetu kupata mielekeo yao kuhusu lugha ya Kiswahili. Wilaya ya Isinya ina tarafa mbili ambazo ni tarafa ya isinya na Kitengela. Tarafa hii ya Kitengela iliweza kuwakilisha wilaya ya Isinya kwa kuwa ndio iliyo na wakazi wengi kutoka jamii mbalimbali kuliko tarafa ya Isinya.

1.6. Yaliyoandikwa kuhusu Mada

Utafiti huu umenuiwa kufanywa kutokana na sababu kuu kuwa lugha ya Kiswahili ni lugha rasmi na lugha ya Taifa nchini Kenya ambapo huwa na majukumu mengi mojawapo ikiwa ni kuwaunganisha watu kutoka makabila au maeneo mbalimbali.

Msanjila na wenzake, (2009) wakieleza kuhusu Lugha ya Taifa wanasema kuwa hutumiwa kama utambulisho wa taifa na kwa sababu hiyo inakuwa na hadhi ya juu na kuheshimiwa na serikali na wanajamii. Hivyo basi katika matumizi rasmi na yasiyo rasmi, lugha hii ya Kiswahili inapaswa kupewa kipaumbele kwa kila hali yaani katika kubuni na kuendeleza fikra na mitazamo yao ya ndani na vilevile hisia za ndani.

Mukhwana na Iribe Mwangi, (2011) wakifafanua majukumu ya Lugha ya Taifa wanasema kuwa Lugha ya Taifa huwaunganisha watu kutoka makabila au maeneo mbalimbali katika taifa ili waweze kushirikiana na kufanya kazi pamoja kwa manufaa ya taifa lao. Ufafanuzi huu umetufaidi katika kutanabahi manufaa ya matumizi ya lugha ya Kiswahili miongoni mwa jamiilugha mbalimbali na itatusaidia kuchunguza mielekeo walio nayo jamiilugha ya Kimaasai kuhusu Kiswahili inayowapelekea kutoitumia katika miktadha rasmi.

Matumizi ya Lugha ya taifa yaani Kiswahili hayatekelezwi kama inavyostahili katika tarafa ya Kitengela kwani lugha ya mama yaani lugha ya Kimaasai hutumiwa mara kwa mara kwa mfano katika mikutano ya wazazi shuleni, ya kisiasa, katika baraza la chifu, katika sherehe mbali mbali kama vile harusi, kufuzu katika shahada mbalimbali na kwenye mazishi. Kutokana na hayo, maswali yaliyotupitikia ni kama vile;

- a) Kwa nini lugha ya Kiswahili ambayo ni rasmi haitumiwi katika mazingira rasmi?
- b) Mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu Kiswahili ni yapi kiasi ya kwamba wao hutumia lugha ya mama yaani Kimaasai zaidi kuliko Kiswahili katika mikutano rasmi?

Kuhusu lugha ya Kiswahili, kuna tafiti kadhaa ambazo zimefanywa zikizingatia mielekeo. Duran (1975), alitaka kubainisha dhima ya Kiswahili katika jamii za mashambani katika muktadha wa wingi-lugha. Matokeo yalionyesha kuwa Kiswahili kilipewa nafasi kubwa kutokana na uwezo wake wa kuleta umoja wa kijamii. Hii ina maana watu wengi walitumia Kiswahili kutokana na mielekeo ya 'kiushirika.' Utafiti wetu ulidhamiria kuchunguza mielekeo ya jamiilugha ya Kimasai kuhusu lugha ya Kiswahili na kutambua sababu zinazopelekea kwa wao kutoipa nafasi kubwa katika mikutano rasmi.

Onyango (1990), alishughulikia mielekeo ya wasomi (wote kwa ujumla) kuhusu matumizi ya Kiswahili katika miktadha rasmi na isiyo rasmi. Katika uchunguzi huo walipata kuwa upeo wake ulikuwa mpana mno. Utafiti wetu ulishughulikia mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu Kiswahili na sababu za wao kuwa na mielekeo hiyo.

Kembo-Sure (1996), alishughulikia mielekeo ya Wakenya kuhusu Lugha ya Kiingereza mintarafu lugha zingine za kienyeji pamoja na Kiswahili. Ilibainika kuwa Wakenya wengi walipenda kujifunza Kiswahili kwani lugha hiyo ni ishara ya umoja wa kitaifa. Kembo-Sure hata hivyo anaeleza kwamba Wakenya walioelimika walipendelea Kiingereza kwa kuwa ndiyo lugha iliyowawezesha watu kupata ajira na kuwawezesha katika mawasiliano ya kimataifa. Kwetu hili ni suala la kimjadala kwani kwa hivi sasa eneo linalotumia Kiswahili ni pana mno kiasi cha kuwa lugha hii inafaa kuitwa Lugha ya Kimataifa katika Afrika Mashariki na Kati. Jambo hili lilitupa motisha kuchunguza mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu Kiswahili kwa kuwa lugha ya Kimaasai aghalabu hutumiwa katika miktadha mbalimbali rasmi na viongozi mbalimbali tarafani Kitengela.

Namulanda (2002), amechunguza mielekeo ya wasikilizaji kuhusu taarifa za habari katika Kiswahili. Uchunguzi huo ulifanywa katika mtaa wa Komarock, Nairobi. Aligundua kuwa wasikilizaji wengi wenye kiwango cha elimu ya kidato cha nne hawakuwa na mielekeo kubalifu ya kusikiliza taarifa za habari kwa Lugha ya Kiswahili. Utafiti wetu ulichunguza mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu Kiswahili katika tarafa ya Kitengela kwa

kuzingatia; kiwango cha elimu, tofauti za umri na jinsia, makazi, kazi anayoifanya mtu, viongozi na lugha inayotumika kanisani.

Mukhwana, (2008) alilenga miji mikuu mitatu ya Kenya:- Nairobi, Kisumu na Mombasa. Tatizo lake lilikuwa kwamba mitazamo kuhusu lugha katika nchi za Afrika huangazwa kama kiini katika sera ya lugha, matumizi ya lugha na kujifunza kwa lugha. Jambo jingine lilikuwa kwamba, watu wana uwezo wa kutumia lugha mbili zilizo tofauti kwa hivyo huwalazimisha watafiti kuwauliza wazungumzaji upendeleo wao katika lugha husika na kutoa sababu za vipendeleo vile. Utafiti wetu wa mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu Kiswahili, ulihusisha pia waliokuwa na umilisi zaidi katika lugha ya Kimaasai ambapo kwa hali hiyo waliweza kueleza mielekeo yao kuhusu lugha nyingine kama vile Kiswahili.

Mohochi (2011), alitafiti mielekeo ya wasomi wa Kiswahili na viongozi wa Afrika Mashariki kuhusu lugha ya Kiswahili. Katika utafiti wake aligundua kuwa lugha ya Kiswahili imeenea na kukua kiasi cha kuweza kupambana na zingine katika ngazi za kimataifa kwenye mfumo wa sasa wa utandawazi lakini anasema kuwa Kiswahili hakiwezi kupata fanaka inavyotarajiwa huko nje iwapo hakitadhaminiwa nyumbani yaani Afrika Mashariki. Anaeleza kuwa bado lugha ya Kiswahili inakumbana na pingamizi nyingi mno na miongoni mwa vikwazo hivyo ni mielekeo ya lugha inayobainika katika jamii.

Watafiti mbali mbali wamechunguza mitazamo kuhusu lugha hali ambayo ilitupa motisha ya kuchunguza mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu lugha ya Kiswahili. Owala (2014),

ametafiti mitazamo kuhusu Kiswahili miongoni mwa wazungumzaji wa Kijaluo kifani cha shule za msingi katika kaunti ya Migori. Uchunguzi wake umeonyesha kwamba lugha ya Kiswahili aghalabu haitumiwi kama inavyostahili katika kaunti hiyo katika diskosi ya jamii na diskosi rasmi, ambapo anaonyesha vikwamizi vinavyochangia hali kama hii kutokea. Utafiti wetu ulifanywa katika tarafa ya Kitengela na ulihusisha viongozi mbalimbali pamoja na wakazi wa tarafa ya Kitengela wa jamiilugha ya Kimaasai ambapo kwa hali ya kujaza hojaji na mahojiano tuliweza kuchunguza mielekeo walionayo kuhusu lugha ya Kiswahili inayosababisha matumizi ya lugha ya mama yaani Kimaasai katika mikutano yao rasmi.

Makala yake yalijikita zaidi katika mielekeo ya viongozi wa Afrika Mashariki na wasomi wa Kiswahili kuhusu nafasi na umuhimu wa Kiswahili. Utafiti wake ulionyesha maswala muhimu yanayochangia ujenzi wa hiyo mielekeo katika jamii ni thamani ya lugha na zoezi la kujifunza lugha ya pili. Matokeo ya utafiti wake yametupa ari ya kuchunguza yanayochangia mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu Kiswahili kutokana na jinsi viongozi tarafani Kitengela wasivyothamini lugha ya Kiswahili wanapohutubia katika miktadha rasmi.

1.7. Msingi wa kinadharia

Utafiti huu ulitumia nadharia jumuishi ya utambulisho iliyoasisiwa na Giles (1979). Giles anafafanua kwamba utambulisho wa mtu au jamii ni mchakato unaoendelea, ambao kimsingi unahusisha vibainishi vingi vinavyodumishwa na jamiilugha ambayo huunda kiini cha utambulisho wa jamii. Lugha hutumika katika mchakato huu kama ishara muhimu ya kuelezea huo utambulisho unaohusika. Msingi wa nadharia jumuishi ya utambulisho

unazingatia fasili ya jamiilugha inayosema “Jamiilugha inaundwa na wale watu wanaojiona na kujitambua wenyewe kuwa wao wanatokana na jamiilugha moja ambayo iko tofauti na jamii lugha nyingine.” (Giles 1979:253). Fasili hii ya jamiilugha bali na kuwa msingi wa nadharia hii jumuishi pia ni msingi wa maana halisi ya utambulisho. Kuna maana mbili halisi ya utambulisho.

Kwanza ni jamiilugha inapojitambua kuwa iko tofauti na jamii lugha nyingine katika masuala ya msingi kama vile utamaduni, mila na desturi, imani mbalimbali, chakula, mavazi, uchumi au siasa. Utambulisho wa aina hii ndio msingi wa jamiilugha kutetea na kudumisha amali za jamii yao. Dhana ya SISI zaidi kuliko WAO au sisi hatufanyi hivyo, asili yetu ni mahali fulani na lugha yetu ni fulani, chakula chetu sisi ni fulani, hudhihirisha ufungamano uliopo baina yao na jamiilugha yao. Uchanganuzi huu umefafanua nadharia jumuishi ya Giles (1979) inayoonyesha jinsi inavyofanya kazi kwa kushirikisha vibainishi mbalimbali vya kijamii na kiisimu. Vibainishi hivi ni kama vile ; lugha, mila na desturi.

Fasili hii ya kwanza ilituwezesha kutambua vibainishi vya utambulisho vya jamiilugha ya Kimaasai vyenye nguvu vinavyosababisha wao kuwa na mielekeo kuhusu lugha nyingine kama vile Kiswahili, ikiwa ni lugha rasmi nchini Kenya inayostahili kutumiwa katika diskosi rasmi.

Maana halisi ya pili ya utambulisho ni kwa wanajamii wenyewe kuthamini lugha yao pamoja na vibainishi vingine vya msingi vinavyofanya wajione wako tofauti na jamiilugha nyingine. Mbali na kuthamini vibainishi kama vile utamaduni, imani mila na desturi, Kihore na wenzake, (2009) wanasema kuwa ni lazima wanajamiilugha wenyewe kuendelea

kudumisha kwa vitendo vibainishi hivyo vya msingi ili utambulisho wao uweze kudumu. Kipengee hiki cha pili kilituwezesha kutambua kuwa jamiilugha ya Kimaasai kwa matendo hudumisha utamaduni wao na lugha yao ya asili iliyobeba amali za jamii yao na kupelekea kuwa na mielekeo kuhusu lugha ya Kiswahili.

1.8. Njia za Utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika tarafa ya Kitengela, Wilayani Isinya Kaunti ya Kajiado ili kubainisha mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu lugha ya Kiswahili. Njia za utafiti zilizotumiwa katika utafiti huu ni pamoja na hojaji za kujazwa na mahojiano ya moja kwa moja. Maswali ya kufuatilia yalitumiwa katika mahojiano ili kuhakikisha kuwa maswali yaliyoulizwa yamejibiwa kikamilifu.

1.8.1. Ukusanyaji na uchanganuzi wa data

Kwa mujibu wa Mugenda na wenzake (1999), data ni kama habari zote ambazo mtafiti anakusanya ili zimsaidie katika utafiti wake. Wanaainisha data kuwili data msingi na data sekondari. Data msingi ni habari ambazo mtafiti atapata nyanjani. Data sekondari wanaeleza kuwa ni habari ambazo mtafiti anatoa kwenye vitabu, nakala na majarida yaani maktabani.

Data msingi ndiyo njia ya ukusanyaji data tutakayotumia katika utafiti wetu ambapo hojaji za kujazwa na mahojiano yatatumiwa. Mtafiti atatumia maswali ya kufuatilia aliyoandaa kwenye mahojiano.

Tarafa ya Kitengela ina wadi mbili zinazoongozwa na viongozi wa kisiasa waliochaguliwa na Walioteuliwa. Kila wadi ina Lokesheni mbili zilizo chini ya uongozi wa chifu. Kwa ujumla kuna Lokesheni nne ambazo ni Ololokitikoshi, Kitengela, Oloosirkon na Sholinke.

Utafiti wetu ulitumia mbinu ya sampuli kusudio. Kwa mujibu wa Best na Kahn (2010), sampuli kusudio humruhusu mtafiti kuteua sampuli ambayo ina wahusika wenye sifa anazoitaka pekee na wale ambao anakisia kuwa watampa majibu anayotaka kutoka kwa sampuli yake. Kulingana na Creswell (2007), sampuli kusudio ni mbinu muhimu ya uteuzi wa sampuli ambayo si ya kubahatisha kwani inampa mtafiti uhuru wa kuteua sampuli kwa kutengemea sifa anazozitafitia katika jumua yake. Naye Lune (2010), anasema kuwa sampuli kusudio haiizingatii ukubwa wa sampuli bali jambo muhimu ni kama sampuli yenyewe inamwezesha mtafiti kupata data ya kutosha itakayoshughulikia suala la utafiti kikamilifu. Kombo na Tromp(2006) nao wana maoni kuwa sampuli kusudio huwa mwafaka kwa mtafiti pale ambapo kundi au sehemu fulani ya sampuli inaaminika ndiyo ina data mwafaka inayoafiki malengo ya utafiti.

Mbinu ya sampuli kusudio ilitufaa katika utafiti wetu kwani tuliweza kuteua sampuli ambayo ilikuwa na wahusika waliokuwa na sifa tulizotaka kama vile kuwa na sifa za uongozi tarafani na pia wenye umilisi wa lugha ya kimaasai. Mtafiti alitumia muda wake kuwafikia watafitiwa kwa namna mbili. Namna ya kwanza aliwafikishia hojaji za kujazwa. Namna ya pili ambayo ilichukua muda mrefu ilikuwa kuwafikia watafitiwa kwa shughuli za mahojiano baada ya kuwasiliana na wao.

Tuliteua chifu wanne, mmoja kutoka kila Lokesheni ambapo walipewa hojaji za kujazwa vilevile na kuhojiwa. Pia manaibu wa chifu wanane yaani wawili kutoka kila lokesheni walijaza hojaji na kuhojiwa. Viongozi wa kisiasa waliochaguliwa ambao ni wawili kutoka katika wadi zote mbili na wawili pia waoteuliwa baada ya uchaguzi, walipewa hojaji za

kujazwa na pia kuhojiwa. Viongozi wanne wa kijiji pia walipewa hojaji za kujazwa na baadaye walihojiwa. Wakazi kumi na sita kwa kuzingatia umri na jinsia kutoka kila Lokesheni walipewa hojaji za kujazwa na pia walihojiwa, pamoja na viongozi wanne wa Kanisa. Kulikuwepo na baadhi ya wakazi waliojaza hojaji na kuhojiwa kwa lugha ya Kimaasai. Kwa ujumla watafitiwa 40 walihusishwa.

Mahojiano yalifanywa ana kwa ana nyanjani katika lokesheni zote nne, ili mtafiti aweze kupata maelezo kwa kina. Kwa kufanya vile mtafiti huweza kupata mambo ambayo hayawezi kuchunguzwa kwa uwazi kama vile hisia, mielekeo, fikra na mengineo. Ujuzi aliutumia mhoji uliwawezesha watafitiwa kutoa ufafanuzi wao kwa uhuru. Majibu yalitolewa kwa kutumia majedwali ya frikwenzi. Viathiriwa kwa ajili ya utafiti huu vilihusu; Tofauti za umri na jinsia, kiwango cha elimu, viongozi, makazi ya mtafitiwa na kazi anayofanya mtu. Mbinu hii ilitusaidia katika uchanganuzi wa data yetu na hata katika utoaji mahitimisho.

Suala la mielekeo kuhusu lugha ya Kiswahili ni la manufaa likifanyiwa utafiti zaidi ili lugha ya Kiswahili iweze kukuzwa zaidi na pia kuiwezesha kutimiza majukumu yake. Mojawapo muhimu ikiwa ni kuwaunganisha watu kutoka makabila au maeneo mbalimbali katika taifa. Utafiti huu ni muhimu kwa kuwa ni hatua ya kuendeleza na kukuza lugha ya Kiswahili. Kiswahili peke yake ndiyo lugha iliyofikia hatua hiyo ya kuwekewa mikakati ya kuendelezwa. Hii ni kwa sababu ni lugha ya kufundishia, lugha ya taifa na lugha rasmi nchini Kenya. Malengo haya ya lugha hii (Kiswahili) yataafikiwa iwapo visababishi vya mielekeo tofauti tofauti katika jamiilugha mbalimbali vitachunguzwa kwa kufanyiwa utafiti ili kujua namna ya kukabiliana navyo katika shughuli za kuendeleza lugha ya Kiswahili.

SURA YA PILI

2.0 Historia ya Maendeleo ya Kiswahili Kajiado

2.1 Utangulizi

Ili kuweza kuzungumzia mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu Kiswahili katika Tarafa ya Kitengela ni muhimu tutangulize kwa kuangalia historia na maendeleo ya Kiswahili katika Kaunti ya Kajiado .Sura hii itakuwa ni msingi wa yale tutakayoyasema baadaye katika kuangalia mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai katika Tarafa ya Kitengela kuhusu Kiswahili. Kama inavyofahamika chimbuko la lugha ya Kiswahili ni upwa wa Afrika Mashariki.Lugha hii haikubaki katika eneo hilo maana, yako mambo yaliyosababisha kuenea kwa Kiswahili kutoka Pwani hadi bara.Mambo hayo ni shughuli za biashara, dini, ukoloni na hatimaye harakati za uhuru (Whiteley, 1969).

Kihistoria, wageni walikuja Pwani ya Afrika Mashariki kwa ajili ya kufanya biashara.Wenyeji wa Pwani walikuwa wakisafiri kwenda bara kwa ajili ya kufanya biashara na watu wa huko kwa kuwa walikuwa wendakati .Wageni walipokuja bara wenyeji waliwaonyesha njia walizotumia na hivyo lugha ya Kiswahili ilienezwa kwa njia hiyo kwa kuwa, ni lugha iliyokuwa ikitumika katika mawasiliano baina ya wenyeji wa Pwani na wa Bara kwa kipindi kirefu hata kabla wageni kuwasili.

Kuenezwa kwa dini za kigeni kama Uislamu na Ukristo vile vile kulichukua nafasi kubwa katika maisha ya wenyeji wa Kajiado na upataji wao wa Kiswahili.Waarabu waliotopea katika dini ya Kiislamu, walitumia Kiswahili. Wahubiri walilazimika kujifunza Kiswahili ili kuelezea mafungu ya Korani kwa lugha iliyoeleweka na wengi ambayo ilikuwa ni

Kiswahili. Kwa upande wa dini ya Kikisto, mwanzoni Wamisionari hawakutaka sana kuitumia lugha ya Kiswahili kwa kuwa waliifananisha na Uislamu. Baadaye walilazimika kutumia Kiswahili kuhubiri ukristo na kuandika maandiko matakatifu.

Viko vipindi vitatu vya ukoloni vilivyokuwa na athari kubwa kwa lugha ya Kiswahili hasa Kajiado. Kipindi cha kwanza kilikuwa ni ukoloni wa Kiarabu. Kipindi hiki kilihusika moja kwa moja na uenezaji wa Kiswahili. Wakati huu misafara ilitoka Pwani kwenda bara na ilitumia Kiswahili kimawasiliano.

Kipindi kilichofuata kilikuwa cha ukoloni wa Kijerumani ambacho kilikuta Kiswahili kimeanza kutumika kwa wingi na hivyo Wajerumani wakaanza kukitumia katika utawala wao. Baada ya Wajerumani, waliofuata walikuwa ni Waingereza. Hawa walifanya kazi kubwa ya kukiendeleza na kukikuza Kiswahili. Azma ya Waingereza ya kufanya vile ilikuwa ni kupata wafanyikazi wa kiwango cha chini. Hawakuruhusu Kiswahili kutumika katika kiwango cha juu. Kwa mujibu wa Kratli na Dyer (2009), katika sehemu kame za nchi ambazo zilimilikiwa na kabila la Wamaasai, haja ya Waingereza ilikuwa kulinda mipaka na kuwazuia wafugaji ambao walihama kutoka sehemu moja hadi nyingine. Huduma za jamii kama vile elimu ambayo ilitumika kusambaza Kiswahili ilikuwa duni sana katika jamii hiyo.

Maelezo mengi yanaonyesha kuwa, kabila la Wamaasai liliwatumia watoto wao kuwachunga mifugo katika harakati za kuhama kutoka sehemu moja hadi nyingine ili kumudu maisha yao. Hali yao ya maisha haikuambatana na mtindo wa elimu uliokuwepo . Ilikuwa vigumu kukubali watoto wao kwenda shule kwani Wamaasai waliamini wangepotea kwa kuacha utamaduni, mila na desturi zao.

Katika kipindi cha kupigania uhuru wa nchi ya Kenya, Kiswahili ndio lugha iliyotumika kuwaunganisha wananchi wote wa Kenya kukiwemo wale wa Kajiado. Wakoloni wa Uingereza walipobaini kuwa Kiswahili kilitumika kama nguzo ya umoja wa Wakenya, walianza kukipiga vita na kushauri lugha za makabila ya Kenya zitumike kama lugha za kufundishia katika shule za msingi kwa lengo la kuvunja umoja wa Wakenya. Hayati Mzee Jomo Kenyatta, rais wa kwanza wa Jamuhuri ya Kenya, alitumia sana Kiswahili wakati wa harakati za kupigania uhuru wa Kenya. Hali hii iliwalazimu Wakenya wote waliotaka kujikomboa kujifunza Kiswahili.

Baada ya kuangazia historia ya maendeleo ya lugha ya Kiswahili nchini Kenya hasa Kajiado, katika kishemu kifuatacho tutaangazia maendeleo ya Kiswahili Kajiado kabla ya uhuru. Hali hii itatupa picha halisi ya hali ya Kiswahili Kajiado na kwa hiyo kutuwezesha kuchunguza mielekeo kuhusu lugha hii katika Tarafa ya Kitengela iliyo katika Kaunti ya Kajiado.

2.2 Kiswahili Kajiado kabla ya Uhuru

Kajiado ni Kaunti iliyo kusini mwa Kaunti ya Nairobi katika barabara kuu ya Nairobi-Arusha. Idadi kubwa ya watu wanaoishi Kajiado ni wa jamiilugha ya Kimaasai. Wamaasai ni wafugaji wa kuhamahama. Kabla ya uhuru biashara ya watumwa ilichangia sana kuenezwa kwa lugha ya Kiswahili na mila ya Waswahili pamoja na dini ya Kiislamu (Kusimba na Kusimba, 2003). Jamii ya Wamaasai haikuwahi kukubali kamwe usafirishaji haramu wa binadamu na wote waliotafuta watumwa walikuwa wakiwaepuka Wamaasai kwa kuwa ni kabila lililopinga utumwa.

Kulingana na Mazrui A. na Mazrui M. (1995), baadhi ya jamii zilizoishi ndani mwa nchi ya Kenya hasa Wamaasai, hazikukubaliana na ujio wa wageni ambao walijishughulisha na biashara na usambazaji wa lugha ya Kiswahili. Jamii ya Wamaasai ilikuwa na sifa za kupenda vita, hivyo basi wakawa kizuizi cha upanuzi wa biashara na usambazaji wa lugha ya Kiswahili katika sehemu walimoishi ikiwepo Kajiado. Mambo mengine yaliyochangia kutosambazwa kwa lugha ya Kiswahili katika eneo hilo ni kuwa, kulikuwepo na vipindi vya vita baina ya Wamaasai na jamii jirani ambao ni Wakamba kwa kuwa imani ya Wamaasai kuhusu mifugo hasa ng'ombe ilikuwa Mungu aliwapa ng'ombe wote duniani kwa hivyo kuchukua mifugo kutoka kwa makabila mengine ni suala la kudai haki yao.

Maisha ya Wamaasai yalikusisha sana ng'ombe. Msingi wao wa chakula ulikuwa maziwa, nyama na damu. Wanyama hao waliwapa pia samadi ya kujengea nyumba zao, ngozi ya kutengenezea mavazi na malazi yao. Malipo kama vile ya mahari au ya mauaji ya mtu wa kabila la Kimaasai yalifanywa kwa kutumia ng'ombe.

Jamiilugha ya Kimaasai haikupenda kujihusisha na shughuli za biashara au uwekezaji katika ardhi kinyume na makabila kama vile ya Wakamba na Mijikenda yaliyopakana na Wamaasai na yalikusika katika biashara huku lugha yao ya kimawasiliano ikiwa Kiswahili. Makabila hayo yaliweza kusambaza lugha ya Kiswahili katika sehemu za bara walikoishi. Thamani kuhusu mila na desturi za jadi za jamiilugha ya Kimaasai kuliwafanya wao kutokupenda mtagusano na jamii yoyote ile (Mazrui.A; Mazrui M.1995). Jamii ya Wamaasai ilienzi lugha yao na utamaduni wao hivi kwamba walidharau jamii zingine na kutozipenda. Walikuwa na imani kuwa wao walitosheleza mahitaji yao kwa kutokushirikiana na jamiilugha nyingine. Kama anavyosema Msanjila na wenzake (2009),

wakifafanua maana ya utambulisho, jamiilugha inapojitambua kuwa iko tofauti na jamiilugha nyingine katika masuala ya kimsingi kama vile utamaduni, mila, desturi na imani hudumisha na kutetea amali za jamii yao.

Jamiilugha ya Kimaasai kabla ya ukoloni kuja Kajiado ilijitenga zaidi na jamiilugha zingine na kupelekea kusambazwa kwa lugha ya Kiswahili iliyokuwa ya kibiashara kwa kiasi kidogo mno. Wamaasai walijishughulisha zaidi na mifugo wao ambapo walihama kutoka sehemu moja hadi nyingine kuwatafutia nyasi kwa hivyo hawakutulia katika sehemu moja wilayani (Ole Katampoi na wenzake 1990). Whitely na Winfred. H (1969), wanasema kuwa Kiswahili kilisambazwa katika sehemu nyingi za Kenya kupitia biashara, utawala, elimu na dini na haya ni masuala ambayo jamii ya Wamaasai haikukubali au kujihusisha nayo sana kwa wakati huo. Baada ya kutathmini hali ya Kiswahili Kajiado kabla ya uhuru, kijisehemu kifuatacho kitaangazia hali ya Kiswahili Kajiado baada ya nchi ya Kenya kujinyakulia uhuru

2.3 Kiswahili Kajiado baada ya uhuru

Nchi ya Kenya ilipojinyakulia uhuru mwaka wa 1963 kutoka kwa ukoloni wa Mwingereza, enzi mpya ya nchi hii iliibuka (Abdulaziz 1972). Hayati rais Mzee Jomo Kenyatta alichukua hatamu za uongozi. Uongozi wa nchi baada ya uhuru, ulikuwa na changamoto nyingi sana kama vile kuleta kwa pamoja makabila mbalimbali yaliyokuwa na mila na desturi tofauti na vilevile yaliyoishi katika sehemu mbalimbali katika nchi, wananchi kuweza kuipenda nchi na kukubali kuwa ni yao na kuwa na utiifu au heshima kwa mamlaka yaliyochukua usukani, Pamoja na hayo, kuliibuka pia suala la lugha na uchanganyaji tamaduni tofauti.

Hata hivyo lugha ya Kiswahili ilithibitika kuwa ya manufaa zaidi katika kuwaunganisha watu. Juhudi zilitiwa na serikali kuendeleza lugha ya Kiswahili hasa katika mfumo wa

elimu. Tume ya kwanza ya elimu iliyoundwa baada ya uhuru katika mwaka wa 1964, mwenyekiti wake akiwa Ominde, ilitia mkazo katika lugha ya Kiswahili kama njia mojawapo ya kufanikisha umoja wa taifa. Tume hiyo ilipendekeza Kiswahili kuwa somo la lazima katika shule za msingi. Kuliwepo vilevile na mapendekezo ya kuanzishwa kwa idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mnamo Agosti 1969, rais Jomo Kenyatta alitangaza Kiswahili kuwa lugha ya Taifa na kubashiri pia kuwa hoja zote rasmi zitajadiliwa katika lugha ya Kiswahili katika siku zijazo (Mbaabu 1988). Chama cha KANU ambacho kilitawala nchini Kenya kilipitisha azimio kuwa mwaka 1974 utakuwa wa kufanya lugha ya Kiswahili lugha rasmi ya taifa kufuatana na mpango uliopitishwa (The East African Standard, April 7, 1970). Kulingana na Gorham (1974) akifafanua maendeleo ya elimu katika kaunti ya Kajiado baina ya mwaka 1963 na 1974, katika historia jamiilugha ya Kimaasai iliyokuwa katika eneo hilo, ilipinga kwa kiasi kikubwa elimu. Dai la huduma hiyo lilianzishwa kimsingi na jamii ambazo hazikuwa za Kimaasai zilizotawala vituo vya kibiashara katika mji wa Ngong na Loitoktok. Sehemu hizi zilikuwa na idadi kubwa ya watu vilevile idadi kubwa ya wanafunzi katika shule zilizoanzishwa kule, hali ambayo iliwezesha elimu kuendelezwa na kusimamiwa vyema katika maeneo hayo mawili.

Katika sehemu za ndani mwa Kaunti ya Kajiado, ambako Wamaasai waliendeleza ufugaji wa mifugo kama ilivyokuwa desturi yao, mfumo wa elimu haukuonyesha hali ya maendeleo. Waliojiunga na shule zilizoanzishwa walikomea katika darasa la tano au kabla ya kufikia darasa hilo. Mawasiliano baina ya walimu na wakuu wa idara ya elimu katika kiwango cha wilaya na tarafa yalikatizwa. Uhusika wa Wamaasai katika shule uliathiriwa na

hitaji la utamaduni pamoja na hali iliyokuwa ya kawaida ya ufugaji na kuhamahama kwao kutoka sehemu moja hadi nyingine kuwatafutia wanyama wao malisho.

Kuunganisha elimu na utamaduni kwa jamiilugha ya Kimaasai kulikuwa kugumu kiasi cha kuwa wazazi hawakukubali kugharamia mahitaji ya elimu ya watoto wao. Wazee wa Kimaasai waliamini kuwa watoto wao wakienda shule watapoteza lugha yao pamoja na utamaduni wao. Wamaasai wachache sana kwa shingo upande, ndio waliojiunga na shule. Hata ingawa kulikuwepo na upanuzi wa elimu ya msingi katika eneo hili lililokuwa likipinga elimu , shule nyingi zilikuwa na ugumu wa kufikia kiwango cha darasa la nne au la tano, kinyume na miji ya Ngong na Loitokitok katika Kaunti hii ya Kajiado ambazo zilikuwa na waliosoma hadi darasa la saba. Sehemu hizi ziliweza kupata usaidizi kutoka kwa wenyeji na usimamizi kutoka kwa wizara ya elimu kwenye kiwango cha tarafa. Mbali na maendeleo katika elimu, biashara zilipanuka na kusababisha kuwepo kwa ongezeko kubwa la watu .

Lugha iliyotumika zaidi katika miji hiyo miwili ilikuwa ni ya Kiswahili kwa kuwa makabila tofauti yaliingiliana katika miji hiyo na lugha ya mawasiliano walioitumia kuendeleza shughuli zao ilikuwa Kiswahili. Kiswahili kilikuwa ni lugha ya elimu na biashara kutokana na hali ya uwililugha (Abdulaziz 1972). Kutokana na jamiilugha ya Kimaasai kutokupendelea elimu na vilevile kutojikusisha kwao na biashara, hali ya Kiswahili ilikuwa chini sana katika Kaunti ya Kajiado baada ya ukoloni kwani lugha ya Kiswahili iliweza tu kutumiwa mijini katika shughuli za biashara na pia katika shule ambazo zilianzishwa katika hiyo miji.

Baada ya kuangazia hali ya Kiswahili Kajiado baada ya uhuru katika visehemu vifuatavyo tutatathmini hali ya Kiswahili Kajiado katika enzi za tawala za marais mbali mbali Kenya. Hali hii itatuwezesha kuchunguza mielekeo kuhusu Kiswahili katika tarafa ya Kitengela iliyo katika kaunti ya Kajiado

2.3.1 Kiswahili Kajiado enzi ya Kenyatta

Maelezo ya jumla kuhusu historia ya kaunti ya Kajiado, yanalenga mabadiliko ya matumizi ya ardhi yanayoendelea hadi wakati huu kwa kufuata sera za serikali na tawala mbalimbali za Kenya huru. Ugavi wa ardhi ya jamii ya Wamaasai katika kaunti ya Kajiado ulifanywa hatua kwa hatua miaka michache baada ya uhuru. Ili kuzuia mmomonyoko wa udongo kutokana na wingi wa mifugo wa Wamaasai na vilevile uhamaji wao kutoka sehemu moja hadi nyingine, serikali ilipendekeza mgao wa ardhi kwa makundi ya Wamaasai katika kaunti hiyo. Baadaye ardhi iligawiwa watu binafsi mwaka wa 1986 hadi 1990 (Grandin 1989).

Ni wazi kuwa kumekuwepo na mabadiliko katika kaunti ya Kajiado kama vile kupotea kwa sehemu za ardhi ya Wamaasai zilipofanywa mbuga za wanyama pori za Nairobi na Amboseli na desturi ya kuhama kutoka sehemu moja hadi nyingine kubadilika kwa kiasi kikubwa. Haya ni kutokana na mabadiliko ya hali ya anga na pia mabadiliko ya njia za kimsingi za kupata riziki. Mabadiliko hayo yalipelekea uhamiaji wa jamii lugha zingine katika kaunti ya Kajiado na kupata makazi yao kwa kununua ardhi. Ni katika misingi hii vilevile ambapo lugha ya Kiswahili iliweza kuanza kujipenyeza na kuenea katika kaunti hii ya Kajiado.

Hadi hivi karibuni, jamii ya Wamaasai iliishi pamoja katika eneo kubwa au boma (manyatta) yenye familia 6 hadi 12 (Jacobs 1965, Njoka 1979). Katika hali hiyo waliweza

kushughulikia malisho ya mifugo wao kwa pamoja. Wakati wa misimu ya kiangazi, Wamaasai walihamia maeneo ambayo hayakukumbwa na hali ya ukame. Ardhi katika kaunti ya Kajiado ilikuwa ya Wamaasai wote bila ya mipaka. Kulikuwepo na uhuru wa kuhamia popote palipokuwepo na malisho bora kwenye Kaunti kwa Wamaasai. Baada ya uhuru mwaka wa 1963, wizara ya kilimo ilitua tume ambayo ingeshauri serikali kuhusu ugawaji wa pamoja na utekelezaji wa mipango kuhusu uhifadhi, usimamizi na matumizi mema ya maeneo ya kuchungia wanyama. Ugawaji ardhi ya Wamaasai, kwa kiasi kikubwa ulimtegemea Brown (1963) kwa utafiti wake uliohusu ushughulikiaji wa matatizo katika maeneo ya kulishia wanyama.

Brown(1963) aliona kuwa maafikio ya kimsingi kuhusu uhifadhi wa eneo la kulishia wanyama ungewezeshwa na kupunguzwa kwa idadi ya wanyama au mifugo, ili maeneo hayo katika kaunti ya Kajiado yaweze kuhimili idadi ya mifugo. Kitendo cha kuhama kutoka sehemu moja hadi nyingine kilifaa kizuiwe kwa uanzilishi wa ulishaji katika maeneo kwa zamu. Alionelea kuwa hayo yangefanikishwa katika maeneo hayo ya ardhi ya umma kwa kuchochea kubuniwa kwa mashamba ya kibinafsi ya kulishia au kuazishwa kwa muungano wa mashirika ya kulisha wanyama yaliyo na maeneo ya ardhi ya kudumu.

Katika mwaka wa 1965, serikali ya Kenya chini ya uongozi wa hayati mzee Jomo Kenyatta ilitoa pendekezo la mradi wa mifugo kwa Benki ya Dunia. Yaliyopendekezwa ni miundo tofauti tofauti ya mipangilio ya jamii na mfumo wa ikolojia katika nchi ya Kenya. Haya yalikuwa ni kwa madhumuni ya kuboresha sehemu muhimu zilizotengwa za mifugo kunywea maji. Mojawapo ya sehemu hizo ilikuwa ni katika kaunti ya Kajiado. Haya yalinuiwa kuwezesha mabadiliko ya maelekezo ya uzalijaji kutoka uchumi wa kijungujiko

hadi uchumi wa kuleta faida kimsingi, kwa kugawa mashamba yaliyolishiwa mifugo kwa makundi ya wenyeji ambao ni Wamaasai. Mashirika ya Umoja wa Mataifa , pamoja na wizara ya kilimo yaliunga mkono na kusaidia katika kutoa orodha ya raslimali ya maeneo ya kuchungia wanyama, mifugo, idadi ya wanyama pori na hali ya maji katika kaunti ya Kajiado ili mipango ya ugawaji wa mashamba ifanywe kwa ukamilifu.

Mwishoni mwa mwaka 1966 mpango huo wa kugawa ardhi ya kulishia mifugo kwa makundi ya wenyeji, ulipitiwa tena ili kubainisha maamuzi kuhusu ardhi kwa kuzingatia pendekezo la mradi wa UNDP (Grandin, E.1991).Wazo la ugawaji wa mashamba kama ulivyopendekezwa na Wizara ya maendeleo ya Kilimo nchini Kenya , ulihusu utengaji wa sehemu za ardhi katika kaunti ya Kajiado na kugawa kwa ranchi na kisha kumilikiwa na kikundi cha watu kilichojiandikisha kama wanachama wa ranchi hizo maalum. Kinyume na awali uhamaji wa mifugo kutoka sehemu moja hadi nyingine uliweza kuzuiwa kwa kiasi fulani kwani uchungaji wa ng'ombe ulifanywa katika ranchi za makundi hayo. Matumizi ya mipaka iliyowekwa ilinuiwa kuwazuia wale wasio wanachama kuwalisha mifugo wao humo. Kupitia njia ya kupewa mikopo kwa wanachama, maendeleo ya ujenzi wa mijengo iliyohitajika katika ufugaji kama vile majosho, ununuzi wa vifaa vilivyohitajika na ununuzi wa ng'ombe wa kulishwa kwa muda kisha wauzwe baadaye ulikuwa jaribio la kubadilisha ile hali ya awali ya ufugaji iwe ya kuleta faida.

Ole Pasha (1981) anafafanua kuwa, wafugaji hasa Wamaasai huwa na desturi ya kushuku mipango, utekelezaji au desturi mpya iliyo kando na jamii yao. Imani yao ni kulinda na kuhifadhi utamaduni, lugha na desturi zao. Mradi wa ugawaji ardhi katika ranchi ulikuwa na wale walioupinga kwa kuwa waliamini kwamba hata ingawa jamii isiyo ya Wamaasai

haikuruhusiwa kuwa katika ardhi ya Wamaasai na wamiliki wa ranchi, jamii hizo zingeweza kujipatia ardhi hiyo kwa njia ya kununua. Hii ni hali ambayo itapelekea kwa ardhi yao kulimwa na kusababisha mmomonyoko wa udongo kama walivyoona katika kaunti jirani ya Machakos. Pia walidai kuwa kuwepo kwa idadi kubwa ya jamii isiyo ya Wamaasai katika kaunti ya Kajiado kutasababisha kupotea kwa utamaduni wao ambao walitaka kuona ukihifadhiwa (Ole Pasha 1986).

Waliounga mkono mradi wa ugawaji wa ardhi katika ranchi za makundi katika kaunti ya Kajiado walionelea ulifaa kwa kuwa ungewaletea maendeleo ya kibinafsi na kuinua hali ya maisha. Pia mradi wa ugawaji ardhi katika ranchi ungewawezesha kupata mikopo kwa kutumia cheti cha umilikaji ardhi na hii ingekuwa mikopo isiyokuwa na masharti kama ushahidi, upunguzaji wa hali ya umaskini na kusaidia jamii ya Wamaasai kuhusika katika kilimo na pia katika urekebishaji wa vifaa na mijengo waliokuwa wakitumia katika ufugaji. Baadaye sehemu zote za Wamaasai katika kaunti ya Kajiado zilikubaliana kuhusu mradi wa ugawaji wa ardhi katika ranchi kwa vikundi (Tazama kiambatanisho cha nane). Mradi huo uliwezesha maendeleo yafuatayo kupatikana katika kaunti ya Kajiado kupitia kwa usimamizi wa serikali iliyotawala ya hayati rais Jomo Kenyatta;

- a. Kuwazuia wachache walioelimika nyakati hizo kujigawia sehemu kubwa ya ardhi kutoka kwa ardhi ya umma. Tishio la kumiminika kwa jamii zisizo za Kimaasai katika kaunti ya Kajiado lilizuiwa.
- b. Mradi wa ranchi kwa makundi ya watu ulianzisha mbinu mpya ya usimamizi wa mifugo na ujenzi wa vifaa kama vile vifaa vya kutumiwa na mifugo kama vya kunywea maji, majosho, visima, mabwawa, matangi na mabomba ya maji.

- c. Mradi huo pia ulichochea ujenzi wa shule, maduka na vituo vya afya.
- d. Wanyama pori waliweza kupata uhuru wa kuendelea kuzururazurura katika sehemu pana za Kaunti ya Kajiado. (Rutten .M, 1995).

Kupitia kwa iliyokuwa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo mbinu mpya za ufugaji zilizinduliwa katika kaunti ya Kajiado. Msanjila na wenzake (2009) wanaeleza kuwa, kwa kuzingatia maendeleo yaliyosababisha maingiliano ya watu duniani ni nadra sana kukuta jamiilugha inayotumia lugha moja tu. Ili jamiilugha ya Kimaasai iweze kuzitumia mbinu hizo, zilihitaji maelekezo ambayo yalipelekea kuwepo na maingiliano ya jamii ya Wamaasai na wataalamu kutoka kwa makabila mbali mbali ambapo mawasiliano yalifanywa katika lugha ya Kiswahili. Kama anavyoeleza Whitely na mwenzake (1969), lugha ya Kiswahili ilisambazwa kupitia biashara na elimu.

Ujenzi wa maduka, shule na pia vituo vya afya kutokana na mradi wa ugawaji wa ranchi kwa vikundi vya Wamaasai pia uliwezesha lugha ya Kiswahili kuenezwa katika kaunti ya Kajiado kwa kuwa ununuzi na uuzaji bidhaa ulifanyika na pia watoto walianza kuhudhuria shule. Mawasiliano katika ununuzi na uuzaji bidhaa, vile vile kwenye vituo vya afya, yalifanywa kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Ufugaji katika ranchi pia ulihusisha mbinu mpya za ufugaji ng'ombe waliokuwa wakiuzwa kwenye soko la mifugo baada ya kunona , hali ambayo iliwahusisha Wamaasai katika biashara ambapo lugha ya Kiswahili ilitumika.

2.3.2 Kiswahili Kajiado enzi ya Moi

Wafugaji wanaozungumza lugha ya Maa huchukua muda kukubaliana na desturi geni (Bersen.1979). Hawapendelei mambo yanayotoka nje ya jamiilugha yao kuigwa au kukubaliwa moja kwa moja bali wao hupendelea maamuzi yao ya kutoka jadi. Wanakamati

walioteuliwa kusimamia ranchi zilizogawiwa makundi ya Wamaasai walipata changamoto nyingi walipofanya kazi ya makundi hayo ya ushirika. Hawakuafikia maazimio yao na mara nyingi walikosa kutekeleza ahadi zao. Vifaa vilivyokuwa vikitumika kwenye ranchi havikusimamiwa vyema wala kufanyiwa marekebisho vilipoharibika. Mipaka kwenye ranchi haikushughulikiwa wala mikopo iliyochukuliwa na wanachama kulipwa. Waliosimamia ranchi hizo walikuwa vijana wenye umri mdogo hali ambayo ilileta utata kwa kuwa kulingana na desturi ya Wamaasai, wazee ndio wanaokubalika kuchukua mamlaka ya uongozi na kutoa maamuzi.

Wazee waliokuwa na mali nyingi kila mara walipinga mambo ya ugawaji ardhi kwa makundi ambapo mara kwa mara hawakuhudhuria mikutano ilipoitishwa. Mzozo kuhusu ranchi kwa makundi ulipozidi na kuleta hali isiyo ya amani kwa makundi hayo, wazo la ugawaji wa ranchi hizo za makundi kwa watu binafsi lilizuka. Wengi walitaka kuwa na mashamba yao binafsi kwa kuwa;

- a. Walitaka kutumia vyeti vyao vya kumiliki mashamba ili wajitwalie mikopo, jambo ambalo halingewezekana katika kikundi.
- b. Hawakuwa na imani na wanakamati walioteuliwa kwa kuwa hawakutimiza ahadi zao.
- c. Idadi ya vijana walioongezeka walitaka kumiliki mashamba yao kuliko kugawiwa na baba zao.
- d. Wengine walihofia kunyang'anywa au kuachwa bila ardhi kwa sababu ya wao kutokuwa na uwezo wa kutawala katika ranchi za makundi.
- e. Waliona heri kujiendeleza kibinafsi kuliko katika kikundi.

Kulikuwepo na baadhi ya Wamaasai ambao walipinga pendekezo la ugavi wa ardhi kuwa ya kibinafsi. Walimini kuwa jamii isiyo ya Wamaasai itapata fursa kwa njia rahisi kujipatia ardhi kwa njia ya ununuzi hali ambayo itawawezesha kuingia katika Kaunti ya Kajiado kwa idadi kubwa na kudhoofisha utamaduni wa Wamaasai. Ilihofiwa na wazee wa Kimaasai kuwa ugawaji ardhi katika sehemu ndogo ndogo utaendeleza ukulima wa mimea na kutokana na hayo, mifugo wataathirika kwa kuwa sehemu ya kuwalishia haitakuwa ya kutosha. Walilalamika pia kuwa ukuzaji wa mazao kwa wingi utasababisha mmomonyoko wa udongo na vile vile kuwa dhaifu na hali hii ambayo ingesababisha nyasi kutokumea.

Katika mwezi wa Aprili mwaka 1989, rais mstaafu Daniel Moi ambaye kwa wakati huo ndiye aliyekuwa mamlakani nchini Kenya aliamua kukomesha mzozo uliokuwa ukiendelea katika kaunti ya Kajiado. Moi alitangaza kuwa wanachama wa kila ranchi walikuwa na haki ya kugawa mashamba yao (Mwangi 1994). Rais Moi alionelea pia kuwa ardhi igawiwe kila mwanachama katika ranchi na awe na cheti chake binafsi cha kumiliki sehemu aliyogawiwa ili kuondoa mzozo katika makundi. Asasi zilizopinga ugawaji wa ranchi za makundi na kuwa ya watu binafsi kama vile idara iliyosimamia ugawaji wa ranchi katika makundi na wizara ya kilimo na ufugaji ziliondolewa katika shughuli za ugawaji ranchi kwa watu binafsi.

Ugawaji wa ranchi zilizomilikiwa na makundi katika kaunti ya Kajiado kwa watu binafsi ulianza katika mwaka wa 1980 ukiungwa mkono na serikali (Kimani, K. 1998). Utekelezaji wa ugawaji ulifanyika mwanzo katika ranchi zilizokuwa karibu na miji mojawapo ikiwa ranchi ya Kitengela ambayo iko karibu na mji wa Nairobi ambao ni mji mkuu wa nchi ya Kenya na pia mji wa Athi River katika kaunti ya Machakos. Ranchi ya Kitengela kwa

wakati huo ilijulikana kama Olkinos (Tazama kiambatanisho cha tisa). Baadaye waliomiliki ardhi binafsi waligawa mashamba yao na kuuza kwa jamiilugha zingine. Ugawaji zaidi katika ploti na kuuzwa uliendelea na kusababisha mwingiliano zaidi wa jamiilugha ya Kimaasai na jamiilugha zingine.

Kutokana na mwingiliano huo, lugha ya Kiswahili ilienezwa hasa katika mawasiliano yaliyotumika kwenye shughuli za uuzaji na ununuzi wa ardhi. Mji wa Kitengela ulianza kupanuka kutokana na majengo ya biashara ambayo yalijengwa na wafanyi biashara na pia ukulima wa mashamba uliendelezwa. Baadhi ya waliouza ardhi zao walianza maisha mapya ya kutowategemea mifugo pekee. Walilima mashamba yao na kukuza mazao hasa mahindi na maharagwe ambapo waliwaajiri wafanyikazi waliotoka katika jamiilugha zingine kuwalimia au wake zao ambao hawakuwa wa kabila la Wamaasai (Njoka 1979).

Wamaasai pia walianza kujenga nyumba zao za kudumu na vile vile majengo ya mifugo wao, na hii ni kutokana na imani walio nayo kuwa mijengo ya kudumu huwawezesha kudai kuwa wamiliki wa sehemu hiyo. Kutokana na kuhudhuria shule kwa watoto wao, waliwapunguza wanyama wao na kuwaajiri wafanyikazi ambao mara nyingine walitoka katika kabila la Wakamba au Wakikuyu na kupelekea kuwepo kwa mwingiliano zaidi wa jamiilugha za Kimaasai walioishi katika sehemu za Kitengela na makabila mengine. Kwa mujibu wa White na Meadows (1981), mradi wa ugawaji ranchi kwa makundi na vile vile kibinafsi umebadilisha njia za ufugaji na hali ya maisha ya Wamaasai. Ununuzi wa mashamba umesababisha ongezeko la idadi ya watu katika kaunti ya Kajiado hali ambayo imefanya jamii ya Wamaasai kuwa na majirani wasio wa kabila lao. Kutokana na hayo,

kumekuwepo na ndoa baina ya wanaume wa Kimaasai na wanawake kutoka makabila jirani kama vile Wakamba na Wakikuyu.

Mabadiliko zaidi katika jamiilugha ya Kimaasai ni kuwa baadhi yao wameweza kukubali kuajiriwa kazi katika miji ya nchini Kenya. Wengine walihusika na biashara ya uuzaji maziwa, shanga na miti shamba. Mabadiliko ya hali ya maisha ya Wamaasai yalisababisha kuenezwa kwa lugha ya Kiswahili kwa kuwa ndiyo lugha iliyotumika katika mawasiliano, ingawa usanifu wake mara nyingi haukuzingatiwa.

Ingawa kulikuwepo mabadiliko hayo, jamii ya Wamaasai haikuacha kuendeleza utamaduni, mila na desturi zao. Walipendelea kutumia lugha yao ya Kimaasai kwa madhumuni ya kuhifadhi utamaduni wao na vile vile wana imani kuwa ndio lugha walioielewa zaidi. Hii ni kutokana na mfungamano uliopo baina ya watu na jamii yao na ndio utambulisho wao ambao unawafanya kujihisi kuwa wako tofauti na jamii nyingine katika masuala ya kimsingi kama vile utamaduni mila na desturi (rejelea Msanjila na wenzake 2009).

2.3.3 Kiswahili Kajiado enzi ya Kibaki na Uhuru

Miji katika kaunti ya Kajiado imeweza kuendelea kupanuka zaidi kwa kuwa biashara mbali mbali zimeanzishwa. Kutokana na kuanzishwa kwa ushirikiano wa nchi huru tatu za Afrika Mashariki na kuanzishwa kwa umoja wa idara za forodha (U I F) January 2005, biashara baina ya Kenya na Tanzania ziliongezeka zaidi. Barabara kuu kutoka Tanzania hadi Athi River ilihitaji kurekebishwa. Makampuni kama vile vya saruji, EPZ, ukulima wa maua na ufugaji kuku pamoja na vichinjio vya mifugo viliongeza nafasi za ajira. Maeneo ya Athi River na Kitengela ambapo barabara hiyo ilipitia yaliendelea kupanuka zaidi. Kwa misingi

hii watu wa tamaduni mbali mbali waliletwa pamoja ambapo lingua franka kwa jina Kiswahili hutumika .

Hali hii inaendana na mawazo ya Iribemwangi na Mukhwana (2011) wanaosema kuwa, Kiswahili ni lugha ambayo hutumika katika kujenga, kuendeleza na hata kudumisha uchumi, biashara na umoja katika taifa la Kenya. Viongozi wa Kenya na Tanzania walikubaliana kuanzisha mradi wa kuboresha barabara kuu kutoka Arusha kupitia Namanga hadi Athi River. Barabara hiyo vile vile imewasaidia Wamaasai katika usafiri wa haraka hadi mijini na kuwapa motisha ya kuendeleza biashara zao. Usafiri wa watalii hadi mbuga ya Amboseli hufanywa kwa kutumia barabara hiyo na lugha ya mawasiliano baina ya watalii hawa na Wamaasai ni Kiswahili.

Katika sekta ya elimu, rais Kibaki alianzisha elimu ya bure kwa shule zote za msingi nchini Kenya mnamo mwaka wa 2003. Kutokana na hayo, wanafunzi wengi ambao hapo awali hawakuweza kumudu mahitaji ya shule walijiunga na shule za msingi. Katika mwaka huo huo, mradi wa hazina ya Ustawishaji wa Eneo Bunge (CDF) ulianzishwa. Pesa hizo zilinuiwa kutumika kuendeleza miradi mbali mbali mashinani, kutimiza ugawaji sawa wa raslimali za maendeleo katika kila eneo la Kenya na kuzuia kutolingana kwa ugawaji kunakosababishwa na siasa za upinzani. Mpango huo uliwezesha ujenzi wa vituo vya afya, elimu na maji katika sehemu zote nchini Kenya pamoja na sehemu za mashambani ambako hakukutuliwa maanani wakati wa kugawa pesa katika bajeti ya taifa (Okungu 2006).

Miradi mingine ya serikali chini ya uongozi wa rais Uhuru Kenyatta ambayo imeleta mwingiliano wa jamiilugha ya Kimaasai na jamii zingine ni uendelezaji bora wa vituo vya afya na ongezeko la vifaa bora. Vituo vya afya vya Kitengela na Isinya vimeendelezwa

ambapo watu kutoka sehemu mbali mbali katika kaunti huvitembelea kwa matibabu ambapo mawasiliano hufanywa kwa lugha ya Kiswahili kutokana na mwingiliano wa makabila tofauti.

Mradi unaoendelea wa ujenzi reli ya gari moshi kutoka Mombasa hadi Nairobi ulioanza mwaka wa 2013 na unanuiwa kukamilishwa katika mwaka wa 2017, umeleta mwingiliano mkubwa kati ya jamiilugha ya Kimaasai na makabila mengine. Baadhi ya Wamaasai wamepata ajira na wengine kulipiwa mashamba yao yaliyopitiwa na reli. Miradi hii ambayo imeweza kuhusisha kaunti ya Kajiado imesababisha mwingiliano wa jamii mbali mbali na jamiilugha ya Kimaasai kwa kuwa yote imechangia maendeleo katika kaunti hii ya Kajiado. Katika maendeleo hayo lugha ya Kiswahili imeenea kwa kuwa hutumika katika mawasiliano kama lugha unganishi na iliyo horomo.

2.4 Hitimisho

Katika sura hii imebainika hali ya lugha ya Kiswahili kaunti ya Kajiado katika nyakati mbali mbali za historia ya Kenya. Awali kabla ya uhuru Wamaasai, kutokana na utamaduni, mila na desturi zao hawakupenda kutagusana na makabila mengine. Wamaasai waliishi pamoja katika boma au “manyatta” huku wakiwategemea mifugo katika kumudu maisha yao. Wamaasai hawa waliwalisha wanyama wao kwa uhuru katika eneo lao la kaunti ya Kajiado bila ya mipaka huku wakihama kutoka sehemu moja hadi nyingine kulipokuwa na hali ya kiangazi. Wamaasai hawakupenda kushirikiana na jamii zozote kwa kuwa waliamini kuwa kwa kufanya vile utamaduni wao ungepotea, kupotoshwa au kutiwa najisi.

Mradi wa ugawaji ranchi katika makundi ulipoanzishwa na rais wa kwanza Mzee Jomo Kenyatta, makundi ya Wamaasai yalimiliki ranchi hizo kwa pamoja na kuzisimamia. Mradi

huo ulipokosa kutimiza ahadi zilizoahidiwa, Wamaasai walionelea ilikuwa bora shamba zigawiwe watu binafsi kwa kuwa walihofia shamba zao zingevamiwa na watu kutoka makabila mengine au kuchukuliwa na serikali.

Watu binafsi walipomiliki sehemu zao za shamba baada ya rais Moi kutoa wito huo ili kukomesha mzozo, Wamaasai walianza kuuza sehemu za shamba zao kwa watu wa makabila mengine na hapo ndipo mwingiliano wao na makaila mengine ulianza. Kutokana na huo mwingiliano, lugha ya Kiswahili ilianza kuenea kwa kasi katika kaunti ya Kajiado.

Miradi iliofuata katika kaunti ya Kajiado chini ya uongozi wa marais Kibaki na Uhuru iliwezesha kupanuka zaidi kwa miji na kuendeleza mwingiliano zaidi wa jamiilugha ya Kimaasai na jamiilugha zingine. Maisha ya jamiilugha ya Kimaasai yamebadilika tangu miji hiyo ipanuke kwa kuwa hukuza mazao ya shambani pia wamepunguza kuhamahama kama walivyofanya awali na kupata nafasi ya kuwajibika katika biashara kama vile ya kuuza na kununua ng'ombe, kuuza maziwa, shanga pamoja na dawa za kienyeji. Mwingiliano huu ulifanyika hatua kwa hatua na umesababisha kuenea kwa lugha ya Kiswahili katika kaunti ya Kajiado kwa kuwa ndiyo lugha ya mawasiliano mapana hasa mijini.

Hata hivyo, jamiilugha ya Kimaasai bado inashikilia mila na desturi zao kwa kuwa haitaki kupoteza uasili wake. Tukizingatia mafungamano yaliyopo baina ya lugha na utamaduni, lugha ya Kimaasai bado ni maarufu miongoni mwa watu hawa.

Baada ya kuangazia jinsi lugha ya Kiswahili ilivyoanza kuenea katika kaunti ya Kajiado, katika sura ifuatayo tutajadili mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu lugha ya Kiswahili katika tarafa ya Kitengela wilayani Isinya kaunti ya Kajiado.

SURA YA TATU

3.0 Uchanganuzi wa Data

3.1 Utangulizi

Katika sura hii mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu Kiswahili katika tarafa ya Kitengela wilayani Isinya kaunti ya Kajiado imejadiliwa. Sampuli kielelezo ni lokesheni nne katika tarafa ya Kitengela zikiwa ni lokesheni ya Kitengela, Oloosirkon, Sholinke na Oloolotikoshi. Walengwa katika utafiti huu walikuwa viongozi wa kisiasa waliochaguliwa na walioteuliwa, machifu na manaibu wao, viongozi wa vijiji na wakazi wachache ambao tuliwateua kimakusudi kwa kuzingatia umri na jinsia. Watafitiwa hawa waliteuliwa kwa sababu wengi wao huhusika sana katika miktadha rasmi. Sura hii ya tatu inawasilisha na vilevile kuchanganua data tuliyopata katika kushughulikia mada yetu ya utafiti.

3.2 Watafitiwa katika utafiti

Jumla ya wakazi kumi na sita wa jamiilugha ya Kimaasai kutoka lokesheni nne tarafani Kitengela walihusika katika utafiti huu. Wao walikuwa watafitiwa wanane wa jinsia ya kike na kiume ambao waliwakilisha kila lokesheni tarafani na wenye umri kati ya miaka 18 na 30. Walijaza hojaji na pia kuhojiwa. Kulikuwepo pia na wanane waliokuwa na umri wa zaidi ya miaka 30 na wa jinsia ya kiume na kike. Katika hao wanane ambao walikuwa na umri mkubwa, watatu hawakuweza kusoma. Walihusishwa katika mahojiano ya moja kwa moja na walipendelea mahojiano katika lugha ya Kimaasai. Watano walijaza hojaji kwa kutumia lugha ya Kimaasai na vilevile walihojiwa kwa lugha hiyo hiyo. Viongozi wa kisiasa

waliochaguliwa walikuwa wawili na pia wawili ambao ni wateuliwa baada ya uchaguzi nchini na walihusika katika kujaza hojaji na pia kuhojiwa.

Viongozi wanne wa vijiji kutoka katika lokesheni zote nne tarafani Kitengela walihojiwa na pia kujaza hojaji. Machifu wanne ambao waliwakilisha lokesheni wanazoongoza walijaza hojaji na kuhojiwa. Manaibu wa chifu wanane waliwakilisha lokesheni zao ndogo na walijaza hojaji. Wahubiri wanne pia walihojiwa na kujaza hojaji. Kwa ujumla sampuli kielelezo ilihusu watu arobaini. Sampuli iliyotumiwa ilikuwa sampuli ya kimakusudi. Viathiriwa kwa ajili ya utafiti huu vilihusu tofauti za umri na jinsia, makazi, kazi anayofanya mtafitiwa, viongozi, lugha inayotumika kanisani na kiwango cha elimu.

Hojaji zote ziliweza kujazwa kwa kuwa waliokuwa na changamoto walielekezwa. Watafitwa wote walihusika katika mahojiano ambapo kutumia maswali ya kufuatilia ili kupata mielekeo yao hasa kuhusu lugha ya Kiswahili. Katika mahojiano tuliweza kutumia muda mfupi wa kati ya dakika ishirini na thelathini ili kuzuia kutumia muda wao mwingi. Kama jinsi Wendo (2009), anavyoeleza kuwa lugha ya Kiswahili huchukuliwa na wengi kuwa ni lugha ngumu kuelewa msamiati wake, baadhi ya watafiwa walijaza hojaji huku wakiongozwa kwa kuwa walidai kuwa lugha ya Kiswahili ni ngumu.

Jedwali 3.1 Jumla ya walengwa katika utafiti na jinsia

Walengwa	Kike	Kiume	% Kike	% Kiume
Wahubiri	1	3	25	75
Wakazi	8	8	50	50
Viongozi wa kisiasa waliochaguliwa na walioteuliwa	2	2	50	50
Machifu	0	4	0	100
Manaibu wa chifu	0	8	0	100
Viongozi wa vijiji	2	2	50	50
Jumla	13	27		

Wakazi waliolengwa katika kila lokesheni ni wawili na walio na umri kati ya miaka 18 na 30, jinsia ya kike na kiume, vilevile wawili walio na umri zaidi ya miaka 30 na wa jinsia ya kike na kiume. Kwa ujumla wakazi wanane wa jinsia ya kike na wanane wa jinsia ya kiume kutoka lokesheni zote nne walihusika .Yaani, asilimia 50 wa kike na asilimia 50 wa kiume.Wahubiri wengi walionekana kuwa wa jinsia ya kiume. Hata hivyo lokesheni moja ilikuwa na mtafitiwa mmoja aliyekuwa wa jinsia ya kike na kuwakilisha asilimia 25 nao wahubiri wa kiume wakawa asilimia 75.

Viongozi wawili wa kisiasa waliochaguliwa na wananchi katika wadi zote mbili tarafani Kitengela ni wa jinsia ya kiume na wanawakilisha asilimia 50. Wawili vilevile walioteuliwa baada ya uchaguzi nchini na ambao walihusika katika utafiti wetu walikuwa wa jinsia ya kike na wao pia waliwakilisha asilimia 50. Machifu wanne walio viongozi wa lokesheni nne

za tarafa ya Kitengela wote ni wa jinsia ya kiume .Waliwakilisha asilimia 100. Manaibu wa chifu wanane yaani wawili kutoka kila lokesheni walikuwa wote wa jinsia ya kiume na kuwakilisha asilimia 100.

Kulingana na utamaduni wa jamiilugha ya Kimaasai uongozi uliaminika kuwa ni wa jinsia ya kiume. Hali hiyo imeweza kudhihirika katika idadi ya viongozi wa jinsia ya kike katika tarafa ya Kitengela. Hapo awali jinsia ya kike haikupewa fursa ya uongozi wowote ule. Kutokana na mabadiliko yaliyoletwa hasa na elimu na katiba mpya Kenya jinsia ya kike imeanza kupewa fursa ya kuongoza hata ingawa kwa kiasi kidogo sana. Katika utafiti wetu viongozi watano wa jinsia ya kike ndio walioweza kuhusika ilhali wa jinsia ya kiume walikuwa kumi na tisa.

3.2.1 Vipengee vilivyotafitiwa

Vipengee vilivyotafitiwa ni pamoja na tofauti za kiumri na jinsia, makazi, kazi aifanyayo mtu, lugha inayotumika kanisani, viongozi na kiwango cha elimu.

3.2.2 Kipengee cha tofauti za kiumri na jinsia

Waliokuwa na umri kati ya miaka 18 na 30 walionyesha ustadi mwingi katika kujaza hojaji kwa kutumia lugha ya Kiswahili na vilevile katika mahojiano hasa kwa kuzingatia matamshi. Wengine waliweza pia kuchanganya lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Hii ni kwa sababu wao hutagusana na jamiilugha zingine wanapokuwa wakiendelea na masomo kwa wanaosoma na wengine pia wakiwa kazini, hali ambayo huwafanya kuzungumza lugha zingine kama vile Kiswahili na Kiingereza katika mawasiliano mbali na lugha ya Kimaasai.Wao walionekana wakiwa huru wakizungumza lugha ya Kiswahili kwa kuwa ni lugha mara kwa mara huitumia na marafiki zao na wengine huitumia nyumbani

kwa mawasiliano. Kutokana na mahojiano na pia kujaza hojaji, waliokuwa na umri baina ya miaka 18 na 30 walikuwa na mielekeo chanya.

Watafitiwa waliokuwa na umri zaidi ya miaka 30 walilalamika kuhusu jinsi lugha ya Kiswahili inavyoendelea kuchukua nafasi ya lugha ya mama kwa kuwa wajukuu wao na pia vijana wengi huitumia kama lugha yao ya kwanza. Walichukulia lugha ya Kiswahili kama lugha ya kupotosha na kuangamiza mila na desturi za Wamaasai. Kulikuwa na waliopendelea mahojiano katika lugha ya Kimaasai hasa waliokuwa na umri wa zaidi ya miaka 35. Walionelea kuwa Kimaasai ndio lugha walioweza kujieleza vyema kwayo na kuelewa zaidi. Waliamini kwamba lugha ya Kiswahili ni lugha ya Waswahili na vilevile lugha iliyostahili kutumiwa katika mawasiliano mijini wanapowasiliana na makabila mengine. Wengi wao walikuwa na mielekeo hasi kuhusu Kiswahili na kuona kuwa lugha yao ya kiasili ndio iliyofaa kutumiwa katika kuhutubia mikutanoni. Haya yalidhihirika katika swali la 7(a) lililokuwa kama ifuatavyo katika hojaji za kujaza.

7(a) Kwa maoni yako ungependelea viongozi katika tarafa hii kutumia lugha gani wanapohutubia mikutano ya hadhara?

Majibu ya waliokuwa na umri mkubwa yalikuwa kwamba walipendelea lugha ya Kimaasai kwa kuwa ndio lugha yao na walioielewa zaidi inapotumiwa kufafanulia mambo. Vijana walipendekeza lugha ya taifa yaani Kiswahili kutumiwa kwa kuwa ndio lugha iliyoeleweka na makabila yote.

Kufuatana na mila na desturi za kabila la Wamasai, jinsia ya kike hufuata amri za waume zao. Kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili, haikupendelewa pia na watafitiwa wa jinsia ya kike wenye umri mkubwa kwa kuwa walizingatia amri za waume zao kuhusu matumizi ya

lugha ya Kimaasai katika mawasiliano nyumbani na kusesitiza walichopenda waume zao. Wale wa jinsia ya kike pia waliokuwa na umri chini ya miaka 30 hawakuzungumza lugha ya Kiswahili kwa uhuru kama wenzao wa jinsia ya kiume waliokuwa na umri huo hata ingawa pia walipendekeza viongozi kutumia lugha ya taifa wanapohutubu kwenye mikutano.

Jedwali 3.2 Majibu kutokana na kipengee cha tofauti za jinsia na umri.

Umri	Jumla	Idadi chanya	% chanya	Idadi hasi	% hasi
Kati ya miaka 18 na 30	20	16	80	4	20
Zaidi ya miaka 30	20	6	30	14	70

Asilimia kubwa ya watafitiwa walio na umri zaidi ya miaka 30 walionea fahari mazungumzo katika lugha ya Kimaasai ikiwa ni njia ya kuhifadhi lugha yao, utamaduni, mila na desturi kwa kuitumia katika mazungumzo. Kulingana na watafitiwa walio na umri kati ya miaka 18 na 30, asilimia kubwa ilionea fahari mazungumzo katika lugha ya Kiswahili. Walipendekeza lugha ya Kiswahili kutumiwa katika hotuba kama ilivyo jukumu la lugha ya taifa kuwaunganisha watu.

3.2.3 Kipengee cha kazi aifanyayo mtu

Kulingana na utafiti huu, kazi anayoifanya mtu husababisha kuwepo na mielekeo kuhusu lugha ya Kiswahili. Haya hutokana na hali ya mazingira ya mahali pa kazi kwa kuwa huwepo na mwingiliano wa jamiilugha mbalimbali hali ambayo husababisha Kiswahili

kutumiwa katika mawasiliano. Lugha ya Kiswahili ndiyo ambayo hutumika sana kwa mawasiliano katika biashara mbalimbali mijini (Mukhwana 2014). Baadhi ya wakazi wa tarafa ya Kitengela hufanya biashara mbalimbali kama vile uuzaji wa maziwa, uuzaji na ununuzi wa mifugo, uuzaji wa miti shamba, shanga, mavazi yaliyotiwa au kutengenezwa kwa shanga, biashara za sokoni na maduka. Katika shughuli hizi lugha ya Kiswahili hutumika sana ili kufanikisha biashara zao. Mbali na biashara, wanaofanya kazi za kiserikali na pia katika makampuni huona kuwa lugha ya Kiswahili huwawezesha kufanya kazi kwa umoja. Ukubalifu wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mahali pa kazi ulidhihirika wazi katika majibu yao ya swali la 9 katika hojaji.

9)Ukiwa kazini wewe hutumia lugha gani?

Wengi walionyesha kuwa iliwapasa kutumia lugha za Kiswahili na Kiingereza kwa kuwa wanaofanya kazi na wao sio wa jamiilugha ya Kimaasai pekee. Hata hivyo kunao walioyaonea fahari matumizi ya lugha ya Kimaasai wanapowasiliana na wenzao wa lugha ya Kimaasai kwa kuwa huamini wao huelewana vyema zaidi katika biashara.

Jedwali la 3.3. Majibu kutokana na kazi aifanyayo mtu.

Jumla	Idadi hasi	%Hasi	Idadi chanya	% Chanya
40	10	25	30	75

Kutokana na jedwali hili ni bayana kuwa mielekeo ya wakazi wa tarafa ya Kitengela kuhusu Kiswahili kutokana na kazi aifanyayo mtu ni chanya. Kupitia kwa mahojiano na majibu ya hojaji, asilimia 75 ya watafitiwa wafanyao kazi mbalimbali kama vile za kiserikali na

biashara wana mielekeo chanya kwa kuwa lugha ya Kiswahili ndiyo waitumiayo sana katika mawasiliano mahali pao pa kazi

3.2.4 Kipenge cha makazi

Tarafa ya Kitengela kama tulivyoona hapo awali ina lokesheni nne ambazo ni Oloolotikoshi, Kitengela, Sholinke na Oloosirkon. Mji wa Kitengela upo katika lokesheni mojawapo ndogo ya Kitengela. Lokesheni zingine tatu ziko mbali kidogo na mji wa Kitengela lakini zote zina vituo vidogo vya kibiashara vinavyopatikana humo. Lokesheni ndogo ya Kitengela ina wakazi wengi ambao siyo wa jamiilugha ya Kimaasai kinyume na lokesheni zingine tarafani. Kutokana na hali hii lugha inayotumiwa na wakazi humo ni lugha ya Kiswahili kwa sababu ya mwingiliano wa jamiilugha ya Wamaasai na makabila mbalimbali yanayopatikana karibu na pia katika kituo hicho cha kibiashara.

Wakazi walio mbali na vituo vya biashara walipendelea kutumia lugha yao ya kiasili kutika shughuli zao mbalimbali kwa kuwa watu kutoka jamiilugha zingine ni wachache sana. Utafiti wetu ulionyesha kuwa mazingira ya makazi ya watafitiwa yalichangia kuwepo kwa mielekeo hasi na chanya kuhusu Kiswahili kutokana na lugha iliyopendelewa kutumiwa. Vijana wanaoishi karibu na vituo vya biashara wana mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili. Wao hupendelea kutumia lugha ya Kiswahili na huwa na uhuru wa kuchanganya na lugha za Sheng na Kiingereza kinyume na lugha ya Kimaasai ambayo ni vigumu kuichanganya na lugha zingine. Vijana hao walikuwa tofauti na wakazi walioko katika sehemu za mashambani katika tarafa ya Kitengela.

Jedwali 3.4 Majibu kuhusu kipengee cha makazi

Makazi	Jumla	Idadi hasi	%hasi	Idadi chanya	%chanya
Mbali na mji	20	15	75%	5	25%
Karibu na mji	20	4	20%	16	80%

Jedwali hili linadhihirisha kuwa wakazi walio karibu na mji wana mielekeo chanya kuhusu Kiswahili kutokana na mwingiliano wao na jamiilugha zingine hali ambayo hupelekea lugha ya Kiswahili kutumiwa mara kwa mara. Katika mahojiano na kujaza hojaji, wakazi wanaoishi karibu na mji au vituo vidogo vya biashara tarafani hawakuwa na changamoto nyingi katika kujibu maswali katika lugha ya Kiswahili kwa kuwa ni lugha walioitumia wakati mwingi. Wakazi wa mbali na mji au vituo vidogo vya biashara hutumia lugha ya kimaasai mara nyingi katika mawasiliano kwa kuwa walio jirani zao wengi ni wa jamiilugha ya Kimaasai hivyo basi lugha ya kimaasai ndiyo hutumiwa mara kwa mara.

3.2.5. Kipenge cha kiwango cha elimu

Jamiilugha ya kimaasai kufikia sasa iko katika mstari wa mbele kuunga mkono elimu kwa kuwa asilimia kubwa ya vijana imepata elimu hadi kiwango cha vyuo vikuu. Katika utafiti huu, walio na kiwango cha chini cha elimu walionea fahari lugha na utamaduni wao kwa kuwa walipendeleza kuwa ilikuwa bora zaidi kuhifadhi uasili wao. Matumizi ya Kiswahili kutumika kama lugha rasmi nchini Kenya kama ilivyo katika swali la 6(a) yaliugwa mkono kwa wingi na wale waliokuwa na kiwango cha juu cha elimu kuanzia darasa la nane na zaidi. Swali lilikuwa hivi;

6(a) Katika maoni yako kuna manufaa ya Kiswahili kutumika kama lugha rasmi nchini Kenya? (sema ndio au la).

Walio na kiwango cha juu cha elimu hupata fursa ya kutagusana na watu kutoka katika jamiilugha mbalimbali katika sehemu mbalimbali wanakosomea au mahali pao pa kazi ambapo mara nyingi hutumia lugha za Kiswahili na Kiingereza. Baadhi ya wale walio na umri wa miaka 46 na zaidi walipata elimu yao ya msingi katika madarasa ya chini katika lugha ya kimaasai kisha kufikia darasa la tano au sita wengi wao hawakuendelea na masomo yao kutokana na uamuzi wa wazazi wao. Wale wa jinsia ya kiume walihitajika kushughulika malisho ya mifugo na wale wa jinsia ya kike waliozwa .Wengine pia hawakupewa fursa ya kusoma kwa kuwa walipokuwa na umri mdogo wazazi wao hawakuona haja ya elimu. Waliona kuwa kwa kuwasomesha wangepoteza lugha na mila zao na kwa hivyo maoni yao ni kuwa lugha ya Kimaasai inapaswa kutumiwa katika mikutano kwa kuwa ni lugha yao na inapaswa kuhifadhiwa. wao walionyesha mielekeo hasi kuhusu Kiswahili.

Jedwali 3.5 Majibu kutokana na kipengee cha kiwango cha elimu.

Jumla	Idadi chanya	%chanya	Idadi hasi	%hasi
40	25	62.5	15	37.5

Asilimia 62.5 ya watafitiwa ina mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili kutokana na kiwango cha elimu. Wao waliona kuwa ni lugha ya taifa na watu wengi huweza kuelewa. Hata wengi walikuwa na mielekeo chanya. Asilimia 37.5 ya watafitiwa ilionelea lugha ya asili itumiwe mara nyingi kwa kuwa ilidumisha mila na desturi za Wamaasai.

3.2.6 Kipengee cha lugha inayotumiwa kanisani

Nilishughulikia kipengee hiki kwa kuwapa hojaji za kujaza wahubiri wanne kutoka katika lokesheni nne tofauti za tarafa ya Kitengela na pia niliweza kuwahoji. Utafiti ulionyesha kuwa lugha ya Kimaasai ndiyo iliyotumiwa zaidi kuliko Kiswahili katika kusoma Biblia, kuhubiri na pia katika nyimbo za dini. Haya ni kutokana na majibu ya swali la 8 na 9 ambayo yalisoma ifuatavyo katika hojaji za kujazwa zilizopewa wahubiri na pia wakazi:

8(a) Je wewe hupendelea kutumia Biblia ya lugha gani unapohubiri, ya Kiswahili Kiingereza au Kimaasai?

(9) Kwa maoni yako waumini wa kanisa lako hupendelea kuimba nyimbo za dini zilizo katika lugha gani?

Haya pia ni kutokana na swali la 8 kwenye hojaji za kujazwa zilizopewa wakazi ambalo lilisoma hivi;

(8) Kwa maoni yako, kuna manufaa ya lugha ya Kimaasai kutumika katika kuhutubia wananchi na pia kanisani?

Majibu ya asilimia kubwa ya wahojiwa yalikuwa kwamba kwa kutumia Biblia ya lugha ya Kimaasai yaliwawezesha kupata ufafanuzi mzuri na waliweza kuelewa maandiko zaidi kuliko katika lugha ya Kiswahili. Nyimbo za dini pia zilipendelewa kuimbwa kwa Kimaasai. Wahubiri wengine walidai kuwa wanapohubiri au kufundisha, wao huwa na mtu wa kutafsiri kwa lugha ya Kiswahili ili Wakristo wasio wa jamiilugha ya Kimaasai wasiwachwe nje.

Jedwali 3.6. Majibu kutokana na kipengee cha lugha inavyotumika kanisani

Jumla	Idadi chanya	%chanya	Idadi hasi	%hasi
40	15	37.5	25	62.5

Kutokana na yaliyomo katika jedwali hili, asilimia 62.5 ya watafitiwa wanakubaliana ya kwamba lugha ya Kiswahili haitumiwi sana katika nyimbo na mahubiri kanisani jinsi lugha ya Kimaasai inavyotumiwa. Wengi walionyesha mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kimaasai na hasi kuhusu lugha a Kiswahili.

3.2.7 Viongozi

Viongozi mbalimbali walihusika katika utafiti wetu. Wengi wao walikiri kutumia lugha ya Kimaasai wanapowahutubia watu kwa kuwa wao huweza kujieleza vyema kwa lugha ya mama. Wakazi wa Kitengela pia, hasa wa umri mkubwa, walipendelea viongozi wao kutumia lugha ya asili kwa madai kuwa waliielewa zaidi. Vilevile kulingana na desturi ya Wamaasai, ni ishara ya upotovu kuwahutubia wenyeji na pia watu walio na umri mkubwa kwa lugha ya Kiswahili. Walionyesha pia kuwa lugha ya Kimaasai ndio iliyoeleweka vyema.

Wanasiasa waliochaguliwa na walioteuliwa walipendelea kutumia lugha ya Kiswahili wanapowahutubia watu katika maeneo karibu na mji wa Kitengela kwa sababu ya kuwepo kwa watu wengi wa jamiilugha zingine mbali na wale wa Kimaasai. Viongozi waliotafitiwa walionyesha mielekeo chanya kuhusu Kiswahili katika kujaza hojaji na mahojiano kwa kuwa walielewa manufaa ya lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa na lugha rasmi lakini

katika utekelezaji ilikuwa ni kinyume kutokana na kuwa kielelezo kama viongozi katika kuhifadhi lugha, utamaduni, mila na desturi za jamii yao.

Jedwali 3.7 Majibu kutokana na kipengee cha viongozi

jumla	Idadi chanya	%chanya	Idadi hasi	%hasi
40	22	55%	18	45%

Kutokana na majibu ya jedwali hili, asilimia kubwa ya watafitiwa ilikiri kuwa na mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili hata ingawa utekelezaji wake ni wa chini kidogo.


3.3 Muhtasari wa vipengee vilivyotafitiwa

Baada ya kuonyesha matokeo ya vipengee vilivyotafitiwa hapo juu, hapa chini tulieleza kwa kutumia grafu kama jumla ya watafitiwa walioonyesha mielekeo chanya na vilevile watafitiwa walioonyesha mielekeo hasi kuhusu Kiswahili.

Jedwali la 3.8

	Chanya	Hasi
Tofauti za umri na jinsia	22	18
kazi aifanyayo mtu	30	10
Makazi ya mtafitiwa	21	19
Kiwango cha elimu	25	15
Lugha inayotumika kanisani	15	25
viongozi	22	18

Chati 3:1 Majibu kutokana na vipengee vilivyotafitiwa




Chati hii inadhihirisha kuwa kupitia kwa majibu ya watafitiwa, mielekeo yao kuhusu lugha ya Kiswahili iliathiriwa kwa kiasi kikubwa na vipengee vilivyotafitiwa. Viongozi wengi, kwa mfano walionyesha mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili kutokana na wajibu wao wa kuwa kielelezo katika kueleza umuhimu wa Kiswahili kama lugha ya kuwaunganisha watu. Katika matumizi, walipendelea kudumisha mila na desturi ya uasili wao, na utambulisho kama anavyoeleza Tabouret-Keller (1989) kuwa mzungumzaji anapaswa kujiona kuwa yeye ni sehemu ya jamiilugha na mwenye dhamana kwa kuendelea kuitumia lugha yake ili kuidumisha.

Tulitumia nadharia jumuishi ya Giles (1979) katika uchanganuzi wa data. Fasili ya jamiilugha ni msingi wake na vilevile maana halisi ya utambulisho. Maana ya kwanza ya utambulisho imetupa utambuzi wa vibainishi mbalimbali vya kijamii na kiisimu kama vile mila, desturi, utamaduni, imani na lugha ambavyo ndivyo msingi unaofanya jamiilugha ya Kimaasai kutetea na kudumisha amali za jamii yao na vilevile kujitambua kuwa ni tofauti na

jamiilugha nyingine. Kwa kutumia maana halisi ya pili ya utambulisho, tumeweza kubainisha kuwa baadhi ya wanajamiilugha wa Kimaasai hudumisha utamaduni wao na lugha yao ya asili iliyobeba amali za jamii yao ili utambulisho wa jamiilugha yao usipotee.

3.3.1. Uchanganuzi wa data ya walengwa

Katika uchanganuzi, tulichanganua watafitiwa kwa kutumia pai chati au umbo la duara.



Kwa kurejelea pai chati hii tulichanganua jumla ya watafitiwa 40 waliohusika katika utafiti wetu kwa kuzingatia digrii kutokana na jinsi walivyohusika. Uhusika wao ulikuwa wakazi 16 wanane wa jinsia ya kike na wanane wa jinsia ya kiume kwa ujumla digrii 144, manaibu wa chifu 8 digrii 72. Vilevile idadi ya viongozi wa vijiji, wahubiri, wanasiasa na chifu wote ilikuwa 4 kila moja na kuwakilisha digrii 36.

Jedwali 3.9 Mielekezo ya watafitiwa

Uchanganuzi wa mielekezo ya watafitiwa hawa kwa kuzingatia idadi, asilimia na digrii tunapata yafuatayo :

	Watafitiwa	Asilimia %	Digrii
Wakazi	16	40	144
Manaibu wa chifu	8	20	72
Viongozi wa machifu	4	10	36
Viongozi wa vijiji	4	10	36
wahubiri	4	10	36
Wanasiasa waliochaguliwa na walioteuliwa	4	10	36
chifu	4	10	36
Jumla	40	100	360

Kutokana na jedwali 3.9 hapo juu watafitiwa kama jinsi walivyohusika katika utafiti wetu wamebainishwa kwa namna tatu. Idadi yao , asilimia yao na vilevile uhusika wao kwa kuzingatia digrii.


3.3.2 Tofauti za umri na jinsia

Kutokana na data tulioeleza hapo juu, ilidhihirika wazi katika 3.2.2 kwamba asilimia kubwa ya jinsia ya kike na kiume iliyo na umri kati ya miaka 30 na 18 wana mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili kwa kuwa wao huitumia mara kwa mara wakiwa katika shughuli zao kama vile masomoni au kazini na hata pia nyumbani na watoto wao na wafanyakazi wao au wenzao. Kati ya walengwa 20 wenye umri huo wa baina ya miaka 30 na 18, 16

walipendekeza matumizi ya lugha ya Kiswahili kama lugha inayoweza kueleweka na jaiimilugha zote na pia kuwaunganisha na kuonyesha mielekeo chanya hata ingawa wanne walikuwa na mielekeo hasi.

Wengi wa watafitiwa walio na umri wa miaka zaidi ya 30 wa jinsia ya kike na kiume walipendekeza udumishaji wa utamaduni na lugha ya jamiilugha ya Kimaasai kwa kuonyesha kuwa wao huzungumza lugha ya Kimaasai nyumbani na hata wanapokutana katika mikutano. Kati ya walengwa 20 wa umri huo, 14 walikuwa na mielekeo hasi wakati wa majadiliano ilhali 6 walikuwa na mielekeo chanya. Kwa ujumla asilimia 55% ya watafitiwa wote walikuwa na mielekeo chanya na asilimia 45% mielekeo hasi kuhusu Kiswahili.

Chati 3.3 Uchanganuzi wa tofauti za kiumri na jinsia



Matokeo ya utafiti kama yalivyodhihirika katika pai chati 3.3 kwa kuzingatia asilimia na digrii, mielekeo kuhusu lugha ya Kiswahili kulingana na tofauti za umri na jinsia ni chanya na vilevile hasi. Kikundi kikubwa cha wenye umri kati ya miaka 30 na 18 walionea fahari mazungumzo rasmi kwa lugha ya Kiswahili na walio na umri mkubwa walionea fahari


mazungumzo katika lugha asilia. Hii yaonyesha kuwa watu wenye umri zaidi ya miaka 30 bado walishikilia ule uasilia nao wa kati ya miaka 30 na 18 wameathiriwa na mabadiliko kutokana na mwingiliano wao na jamiilugha zingine. Vijana wa jamiilugha ya Kimaasai hutumia, mara kwa mara, Kiswahili au Kiingereza kutokana na shughuli muhimu za kijamii kama vile elimu, kupata kazi baada ya shule, kuendesha biashara, mawasiliano baina yao na vijana wenzao, watoto na wake zao kwa kuwa wengine wameoa kutoka makabila mengine ambayo si ya jamii ya Kimaasai.

3.3.3 Kazi aifanyayo mtu

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, lugha ya Kiswahili ndiyo hutumika sana katika mahali pa kazi. Hii ni kwa sababu jamiilugha mbalimbali huwepo katika pahali pa kazi kama vile katika makampuni au kwenye biashara. Jambo hilo hupelekea kwa lugha inayojulikana na wote kutumiwa kama vile Kiswahili au lugha ya Kiingereza. Asilimia 75% walikuwa na mielekeo chanya kuhusu Kiswahili nayo asilimia 25% walikuwa na mielekeo hasi kwa kuwa walipendekeza lugha asilia kutumiwa wakati ambapo watu wa jamiilugha moja huwasiliana kwa madhumuni ya udumishaji wa lugha yao.

Pai chati iliyopo hapo chini imefafanua mielekeo walionayo jamiilugha ya Kimaasai kuhusu lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia asilimia kwa kutegemea kazi aifanyayo mtu.


Chati: 3.4 Uchanganuzi wa data kuhusu kazi aifanyayo mtu



3.3.4 Makazi

Kutokana na maelezo ya utafiti katika 3.2.4 wakazi wa jamiilugha ya kimaasai ambao makao yao yako karibu na mji au vituo vya biashara walikuwa na mielekeo chanya kuhusu Kiswahili kwa kuwa walitangamana na watu kutoka jamiilugha zingine. Wanaoishi mashambani walikuwa na mielekeo hasi kuhusu Kiswahili kwa kuwa watu wa jamiilugha ya Kimaasai ndio walio wengi hivi kwamba mawasiliano nyumbani hufanywa kwa lugha ya Kimaasai.

Chati 3.5 Uchanganuzi wa data kuhusu Makazi




Pai chati 3.5 inaonyesha kuwa tofauti kati ya waliokuwa na mielekeo hasi na chanya kuhusu lugha ya Kiswahili kwa kutegemea makazi sio kubwa sana kwa kuzingatia asilimia. Asilimia 52.5 walikuwa na mielekeo chanya huku asilimia 47.5 wakionyesha mielekeo hasi.

3.3.5. Kiwango cha elimu

Katika eneo la Kitengela wanajamiilugha ya Kimaasai wachache ndio hawakusoma. Kutokana na kuwa na kiwango cha elimu cha juu na pia wastani, waliokuwa na mielekeo chanya kuhusu Kiswahili wakati wa mahojiano walikuwa asilimia 62.5. Asilimia 37.5 ya wahojiwa na ambao walikuwa na kiwango cha chini cha elimu na vilevile wengine hawakusoma walikuwa na mielekeo hasi.

Chati 3.6 Uchanganuzi wa data kuhusu kiwango cha Elimu




Pai chati 3.6 yaonyesha mielekeo ya watu wa jamiilugha ya Kimaasai kutegemea elimu kwa kuzingatia asilimia.

3.3.6 Lugha inayotumika Kanisani

Kutokana na matokeo ya huu utafiti katika 3.2.6, lugha ya Kimaasai ndiyo hutumiwa sana kanisani katika kuendesha mahubiri na nyimbo za kumsifu Mungu. Asilimia 62.5 ya

wahojiwa wana mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili. Asilimia 37.5 ya watafitiwa wana mielekeo chanya kwa kuwa ndio hutumia lugha ya Kiswahili kanisani hasa wale wanaoishi karibu na mji wa Kitengela. Ipo imani kuwa neno la Mungu huweza kumfikia mlengwa kwa lugha asilia ambayo ni Kimaasai na wala si lugha ya kigeni ambayo katika muktadha huu ni Kiswahili. Pai chati iliyopo hapa chini yadhihirisha mielekeo hii kuhusu lugha ya mahubiri Kitengela.




3.3.7. Viongozi

Kulingana na kishemu 3.2.7 ni dhahiri kuwa asilimia 55% ina mielekeo chanya kuhusu Kiswahili na asilimia 45% ina mielekeo hasi. Tofauti siyo kubwa sana kwa kuwa matumizi ya lugha ya taifa yanaungwa mkono lakini katika utekelezaji ni kinyume. Wakazi wa Kitengela vilevile walionyesha matokeo hasi na chanya kwa kuwa wengi wa wale waliokuwa na umri mdogo walipendekeza hotuba kuendelezwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili ilhali waliokuwa na umri mkubwa walipendekeza lugha ya Kimaasai kutumiwa ili uasilia usiangamie.

Kama ilivyodhihirika katika pai chati iliyopo hapa chini viongozi wengi wa Kitengela hupendelea matumizi ya Kiswahili dhidi ya Kimaasai katika kutoa hotuba zao. Wakiwa

viongozi wa kitaifa wao hawana budi ila kuendeleza sera za serikali kuhusu Kiswahili kama lugha ya taifa na lugha rasmi.

Chati 3.8 Uchanganuzi wa data kuhusu viongozi



3.3.8 Hitimisho

Katika sura hii ya tatu tumewasillisha matokeo ya utafiti wetu kuhusu mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu lugha ya Kiswahili. Matokeo yanaonyesha kuwa wengi wa watafitiwa walionyesha mielekeo chanya kuhusu Kiswahili. Umri kati ya miaka 30 na 18 hupendelea kutumia Kiswahili wakiwa nyumbani. Walio na umri mkubwa walionea fahari mazungumzo katika lugha ya Kimaasai wakiwa nyumbani na vilevile katika mikutano. Lugha ya Kimaasai ilipendelewa kutumiwa ili kudumisha utamaduni, mila na desturi ya jamiilugha ya Kimaasai na pia lugha asilia. Katika sura ifuatayo tumejadili masiala yanayosababisha jamiilugha ya Kimaasai kuwa na mielekeo mbalimbali kuhusu lugha ya Kiswahili kama yalivyojitokeza katika utafiti huu.

SURA YA NNE

4.0 Mjadala Kuhusu Mielekezo Dhidi ya Kiswahili Kitengela

4.1. Utangulizi

Katika sura ya 3 tuliwasilisha data kuhusiana na mielekeo dhidi ya Kiswahili Kitengela na kisha kuichanganua. Katika sura hii tutawasilisha matokeo yanayotokana na ule uchanganuzi wa data ili kudhihirisha mambo ambayo husababisha mielekeo hasi au chanya kuhusu Kiswahili kwa wanajamiilugha ya Kimaasai katika tarafa ya Kitengela wilayani Isinya kaunti ya Kajiado.

Kutokana na uchanganuzi wa data tuliofanya katika sura ya tatu, inabainika kwamba yapo masiala yanayojitokeza na kusababisha mielekeo hasi au chanya kuhusu Kiswahili katika eneo letu la utafiti. Kwa kutaja vipengele tulivyovitafiti tukajadili matokeo.

4.2 Tofauti za jinsia na umri

Kutokana na utafiti tuliofanya, mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu Kiswahili kulingana na tofauti za jinsia na umri ni chanya na hasi. Walio na umri mkubwa hawakukumbana sana na mwingiliano na jamiilugha zingine katika umri wao wa utotoni na ujanani kama walivyo watafitiwa walio na umri kati ya miaka 18 na 30. Hawakuweza vilevile kuhusika sana na elimu, ajira au biashara. Katika malezi yao, lugha ya Kimaasai, utamaduni, mila na desturi za Kimaasai zilizingatiwa sana. Katika mahojiano walionyesha mielekeo hasi kuhusu Kiswahili kwa kuwa waliona ni lugha inayoangamiza lugha ya Kimaasai jinsi miaka zinavyopita. Walidai pia kuwa matumizi ya lugha ya Kimaasai huweza kuthibiti mila na desturi zao. Walionekana kuithamini lugha yao ya asili hivi kwamba waliitaka iweze kudumishwa kwa kutumiwa mara kwa mara.

Walio na umri kati ya miaka 30 na 18 wana mielekeo chanya kuhusu Kiswahili kwa kuwa wao huitumia mara kwa mara katika utekelezaji wa shughuli kama vile elimu, kupata kazi baada ya shule, wakiwa shuleni, kuendeleza biashara na katika mawasiliano baina yao na wenzao au na watoto wao kwa walio na familia. Katika mahojiano baadhi ya walio na umri mdogo walieleza kuwa walitumia lugha ya Kiswahili na pia Kiingereza nyumbani. Nchini Kenya sasa matumizi ya Kiswahili yanaashiria utafu na uzalendo hasa kutokana na vita vya kikabila vya mwaka 2007 / 2008. Matumizi ya Kiingereza nayo ni ishara ya 'usasa' kutokana na hali ya triglossia ipatikanayo Kenya.

4.3. Kazi aifanyayo mtu

Mwingiliano wa jamiilugha ya Kimaasai na jamiilugha zingine zimesababisha mabadiliko mengi katika tarafa ya Kitengela. Mji wa Kitengela umepanuka sana kutokana na shughuli za kibiashara na pia kuhamiwa na wakazi wengi wa jamiilugha zingine. Mabadiliko hayo yamepelekea kuwepo na shughuli za kijamii kama vile biashara, ajira na elimu. Katika kujaza hojaji na mahojiano na watafitiwa, lugha waliokiri kuitumia katika mahali pao pa kazi ni lugha ya Kiswahili ili kurahisisha mawasiliano kwa kuwa ni lugha iliyoeleweka na jamii mbalimbali na kuwezesha upanuzi wa maendeleo.

Mielekeo kuhusu Kiswahili kulingana na kazi aifanyayo mtu ni chanya ingawa asilimia ndogo ilikuwa na mielekeo hasi kwa kuwa walipendekeza matumizi ya lugha ya Kimaasai kuendelezwa wanapowasiliana wao kwa wao. Watafitiwa kama hawa ni watu ambao hawajawahi kutoka kutoka nje ya mipaka ya wanajamiilugha ya Kimaasai wala kuwa na waajiriwa kutoka jamiilugha zingine.

4.4. Makazi

Kutokana na utafiti tuliofanya, makazi ya mtu huwezi kusababisha wao kuwa na mwelekeo hasi au chanya kuhusu Kiswahili. Wanaoishi karibu na vituo vya biashara huweza kuwa na mwingiliano mkubwa mno na watu wa jamiilugha mbalimbali kutokana na ununuzi wa mashamba unaoendelea tofauti na wanaoishi mbali na vituo vya biashara. Matumizi ya lugha ya Kiswahili mara kwa mara, kwa wanaoishi karibu na vituo vya biashara, kulisababisha kwa wao kuwa na mielekeo chanya kuhusu Kiswahili kwa kuwa ndiyo lugha ya mawasiliano baina ya jirani na jirani. Wanaoishi mbali na vituo vya biashara mara nyingi hutumia lugha ya Kimaasai kwa mawasiliano hali ambayo inapelekea wao kuwa na mielekeo hasi kuhusu Kiswahili.

4.5. Kiwango cha elimu

Walio na kiwango cha wastani na chini cha elimu walikuwa na mielekeo hasi kuhusu Kiswahili. Walionelea kuwa ni lugha iliyofaa kutumiwa katika shughuli zingine mbali na nyumbani kama vile kazini na shuleni lakini katika mawasiliano mengine yote lugha ya Kimaasai itumiwe ili kudumisha utamaduni wa Wamaasai. Walio na kiwango cha juu cha elimu walikuwa na mielekeo chanya kuhusu Kiswahili kwa kuunga mkono hoja kuwa ni lugha ya taifa na inayo jukumu la kuwaunganisha watu wa jamii mbali mbali. Walipendekeza pia matumizi ya lugha ya Kiingereza kutokana na hali ya mabadiliko yanayotokea kila uchao kitekinolojia katika ulimwengu kwa jumla.

Ionekanavyo ni kuwa elimu humpa mtu kuwa mwana uwililugha au mwana wingilugha. Hali hii imejitokeza pale ambapo umri wa wale walio na mielekeo hasi kuhusu Kiswahili ni mpevu huku wale walio na mielekeo chanya ukiwa umri mdogo. Wana jamiilugha ya Kimaasai walio na umri wa miaka baina ya 18 na 30 ni wale walioenda skuli. Mfumo wa

elimu Kenya ni hivi kwamba Kiswahili hufunzwa na kutahiniwa na hata kufunziwa. Hali hii ya kufunzwa, kufunziwa na kutahiniwa kwa Kiswahili huwapa wahusika mwono ulimwengu mpana kinyume na wale wazee ambao wanang'ang'ania Kimaasai kutokana na mwono ulimwengu finyu. Si ajabu kwamba mielekeo yao kuhusu Kiswahili ni hasi.

4.6. Lugha inayotumika kanisani

Lokesheni zote nne za tarafa ya Kitengela zina wakazi wanaozungumza lugha tofauti tofauti. Kutokana na mahojiano na viongozi wa kanisa, wakazi wengi walipendelea nyimbo za lugha ya Kimaasai na vile vile muhubiri. Usomaji wa Biblia katika lugha ya Kimaasai ulipendelewa zaidi kwa kuwa walidai maelezo yake yalieleweka kuliko yale ya lugha ya Kiswahili. Baadhi ya wahubiri walidai kuwa na watafsiri katika Kiswahili wanapohubiri na pia walieleza kuwa wao huwa na ujasiri zaidi wanapohubiri na huweza kujieleza vyema kwa kutumia lugha ya Kimaasai. Hali hii inatokana na fikira kuwa mtu hujifunza na kuelewa zaidi akitumia lugha yake asilia iliyo mzaa na kumlea.

Japo watafitiwa wengi walipendelea lugha ya Kimaasai, wapo wachache waliokipendelea Kiswahili. Hawa walikuwa hasa vijana walioelimika. Waliona Kiswahili kama lugha horomo na ilioonyesha 'usasa'. Walijiona na kujihisi Wakenya na wala sio Wamaasai.

4.7. Viongozi

Viongozi wa kisiasa, machifu na manaibu wao na viongozi wa vijijini walikuwa na mielekeo chanya kuhusu Kiswahili lakini walidai kuwa wao hutumia lugha ya Kimaasai mara nyingi wanawapohutubia wananchi ili wenyeji hasa wenye umri mkubwa waweze kuelewa zaidi. Ingawa waliunga mkono matumizi ya lugha ya Kiswahili, walipendekeza

kuchangia udumishaji wa mila na desturi za Wamaasai kama viongozi kwa kutumia lugha ya Kimaasai katika kuhutubia watu.

Viongozi hawa walikipendelea Kiswahili kwa kuwa ni lugha ya taifa na lugha rasmi kikatiba. Wao wakiwa ni wawakilishi wa rais wa Jamuhuri ya Kenya mashinani, hufanya hivyo ili kuendeleza sera ya serikali kuhusu lugha. Wanapotumia Kimaasai huwa vilevile wanazingatia yaliyo katika katiba kuhusu utunzaji na uendelezaji wa lugha ya kiasili ili zisije zikajifia. Yaani matumizi ya Kiswahili na Kimaasai na viongozi ni ishara ya uzalendo lakini katika ngazi tofauti tofauti.

Hitimisho

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, inabainika kwamba jamiilugha ya Kimaasai ina mielekeo hasi na chanya kuhusu Kiswahili. Mielekeo chanya kuhusu Kiswahili kama lugha ya taifa na rasmi nchini Kenya imechangiwa na kuwepo kwa mwingiliano wa jamiilugha ya Kimaasai na jamiilugha zingine na pia utekelezaji wa shughuli muhimu za kijamii kama vile elimu, kupata kazi baada ya shule na kuendesha biashara. Mwelekeo hasi kuhusu Kiswahili ni kutokana na upendeleo wa matumizi ya lugha ya Kimaasai katika mawasiliano kama chombo cha kuhifadhi na kuendeleza utamaduni au uasilia wa Wamaasai. Katika sura ifuatayo, tutaangazia muhtasari wa utafiti huu, hitimisho na mapendekezo kwa watafiti wa baadaye kuhusiana na mada yetu ya utafiti.

SURA YA TANO

5.0 Muhtasari, Hitimisho na Mapendekezo

5.1. Utangulizi

Utafiti huu ulilenga kuchunguza mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu Kiswahili katika tarafa ya Kitengela wilayani Isinya katika kaunti ya Kajiado. Tulichunguza visababishi vya mielekeo hiyo kwa kutumia nadharia jumusishi ya Giles (1979). Fasili ya jamiilugha inayosema kuwa ‘Jamiilugha huundwa na wale watu wanaojiona na kujitambua wenyewe kuwa wao wanatokana na jamiilugha moja ambayo iko tofauti na jamiilugha nyingine’, ilitumika yaani jamiilugha ni msingi wake na maana halisi ya utambulisho.

Kwa kutumia maana ya kwanza na ya pili ya utambulisho tumegundua kuwa jamiilugha ya Kimaasai hujitambua kuwa ni tofauti na jamiilugha nyingine katika maswala ya lugha, utamaduni, imani, mila na desturi. Kwa kuwa vibainishi hivyo hubeba amali za jamii ambazo hudumishwa na utamaduni na lugha asili, ni lazima jamiilugha kudumisha kwa vitendo vibainishi hivyo ili utambulisho wao uweze kudumu. Kutokana na hali hii, jamiilugha huweza kuwa na mielekeo kuhusu lugha nyingine kama wafanyavyo wana jamiilugha ya Kimaasai kuhusu Kiswahili kwani wao huithamini lugha yao na utamaduni wao.

Ili kutimiza madhumuni ya utafiti huu, tulitafuta data ya kimsingi kutoka kwa viongozi mbalimbali na wakazi kwa kuangazia tofauti za umri na jinsia katika lokesheni nne tofauti zilizomo katika tarafa ya Kitengela. Viongozi ndio vielelezo katika kueneza umuhimu wa lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa wanapoitumia katika mawasiliano na

kuwahutubia wananchi. Data ilikusanywa kwa njia ya mahojiano ya moja kwa moja na vilevile hojaji za kujazwa zilitumiwa. Tuligawa kazi yetu katika sura tano.

5.2 Muhtasari

Kwa ujumla, sura ya kwanza ni utangulizi wa kazi hii. Katika sura ya pili, tumeangazia Kiswahili Kajiado kabla ya uhuru, baada ya uhuru na katika enzi za marais walioongoza nchini Kenya hapo awali na aliye hatamuni kwa wakati huu. Aidha katika sura hii ya pili, tumejadili mabadiliko ambayo jamiilugha ya Kimaasai ilipata katika maongozi ya marais mbalimbali. Mabadiliko hayo yalitokea kutoka kwa mwenendo wao wa kuishi kwa kuhamahama kutoka sehemu moja hadi nyingine katika eneo la kaunti ya Kajiado ambapo walimiliki ardhi yote kwa pamoja kisha umiliki wa mashamba katika makundi na umiliki wa mashamba kibinafsi.

Matokeo ya utafiti huu yamewasilishwa katika sura ya tatu. Mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu lugha ya Kiswahili imejadiliwa kwa kuangazia vipengee kama vile tofauti za jinsia na umri, kazi aifanyayo mtu, makazi, kiwango cha elimu, lugha inayotumika kanisani na viongozi. Imebainika kuwa ipo mielekeo chanya na vilevile hasi kwa kutegemea vipengee tulivyovitaja hapo juu.

Sura ya nne imeshughulikia masiala yaliyosababisha mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu Kiswahili. Kutokana na utafiti huu, masiala yaliyojitokeza kuwa kiathiri cha mielekeo ya wanajamiilugha wa Kimaasai ni pamoja na kuthamini lugha yao asilia, harakati za udumishaji wa utamaduni, mila, desturi na pia imani. Walio na umri mkubwa waliona lugha ya Kiswahili ikipiga vita lugha ya Kimaasai kwa kuwa walio na umri mdogo hutumia lugha ya Kiswahili sana katika mawasiliano.

Jambo jingine lililojitokeza katika utafiti huu ni kule kuwa na shughuli mbalimbali za kijamii kama vile elimu, biashara na ajira ambazo zimesababisha kuwepo kwa mwingiliano baina ya jamiilugha mbalimbali na jamiilugha ya Kimaasai na kwa hivyo kuathiri suala la lugha. Masiala haya yameweza kusababisha mielekeo chanya na hasi kwa jamiilugha ya Kimaasai kuhusu Kiswahili.

5.3. Hitimisho

Kwa kuhitimisha, matokeo ya utafiti huu yamedhihrisha kuwa jamiilugha ya Kimaasai katika tarafa ya Kitengela ina mielekeo chanya na hasi kuhusu Kiswahili kutokana na masiala mbalimbali. Kwa kuwa eneo hili ni la wingilugha kwa sababu ya uhamiaji walo na jamiilugha tofauti tofauti na kupelekea kuwepo kwa upanuzi zaidi wa mji wa Kitengela, lugha ya Kiswahili hutumika katika shughuli mbalimbali za kijamii. Mabadiliko ambayo jamiilugha ya Kimaasai imepata kama tulivyojadili katika sura ya pili yamesababisha kuwepo na masiala yanayoonyesha kuwepo kwa mielekeo chanya na hasi kuhusu lugha ya Kiswahili.

Masiala tuliyoyashughulikia ambayo ni pamoja na makazi, umri na jinsia, kazi aifanyayo mtu, lugha inayotumika kanisani, kiwango cha elimu na viongozi yameweza kudhihirisha mielekeo walio nayo jamiilugha ya Kimaasai kuhusu Kiswahili ambayo ni lugha rasmi na ya taifa Kenya. Vilevile yameonyesha matumizi ya lugha asilia ya Kimaasai katika tarafa ya Kitengela.

Mabadiliko katika hali ya maisha ya jamiilugha ya Kimaasai ambayo yanatokea kutokana na mabadiliko yanayoendelea katika ulimwengu yamesababisha mwingiliano zaidi wa Wamaasai na jamiilugha zingine. Wamaasai wameweza pia kujihusisha na shughuli

mbalimbali za kijamii ambazo hazikuwepo hapo awali. Kama anavyofafanua Landweer (2000), umbali wa lugha kutoka kwa mji sio wa kimasafa tu bali pia hupimwa na idadi ya wanajamiilugha ambao mara nyingi huenda wakirudi kutoka mjini kwa shughuli mbalimbali kama vile biashara, kazi na elimu. Kwa njia hii huenda wakafikishia wanajamiilugha walio mbali na mji athari za lugha nyingine.

Wakazi walio na umri mkubwa walikuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili kutokana na kuthamini kwao lugha asilia na pia kutaka kuidumisha. Viongozi wanawapohutubia wananchi hasa katika sehemu za mashambani hulazimika kutumia lugha asilia kwa kuwa ni desturi ya jamii ya Kimaasai kutumia lugha yao wanapokutana katika mikutano ya hadhara na pia ni hali ya kuwaheshimu walio na umri mkubwa. Vijana mara kwa mara hutumia lugha ya Kiswahili na pia Kiingereza katika mawasiliano na katika utekelezaji wa shughuli muhimu za kijamii. Kutokana na matumizi ya lugha hizo katika maeneo muhimu kama vile nyumbani na shuleni, lugha ya Kimaasai katika eneo la tarafa ya Kitengela, inaendelea kufifia na vilevile viwango vyao vya umilisi wa lugha hiyo vimekuwa vya chini.

Wengi walidai kutokuwa na nafasi ya kutumia lugha asilia ya Kimaasai mara kwa mara kwa sababu ya kuwa mbali na nyumbani na pia wafanyikazi wao sio wa jamii ya Kimaasai. Hali hii ilijidhihirisha katika mahojiano ambapo kulitokea mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili na pia Kiingereza na kutokana na kiwango cha juu cha matumizi ya lugha hizi na hata kwa wengine imekuwa ndio lugha ya mawasiliano na watoto wao kwa wale waliooa. Mazingira ya mahali wanapokaa wakazi pia yanadhihisha mielekeo chanya na hasi kuhusu

lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili hutumiwa sana na waishio karibu na mji kuliko wale walio katika sehemu za mashambani.

5.4 Mapendekezo

Kutokana na utafiti wetu, tumetambua kuwa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika tarafa ya Kitengela yanahitaji kufanyiwa utafiti zaidi. Eneo hili linazidi kupanuka zaidi na jamiilugha tofauti tofauti zinazidi kuenea humo hata ingawa jamiilugha ya Kimaasai ndio ya walio wengi. Kwa misingi hii lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha ya taifa inakuwa ni kifaa cha kuzibia mipaka ya kikabila miongoni mwa watu wa makabila mbalimbali tarafani Kitengela. Maendeleo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi yanawezekana zaidi iwapo jamii imeungana kuliko kama imegawanyika. Lugha ya taifa ndio huweza kupigania kuleta umoja huo kwa kuwa kama asemavyo Haugen(1966), huwezesha hali ya jamii mbalimbali kushikamana ndani kwa ndani na kutoingiliwa kutoka nje. Matumizi ya lugha ya Kiswahili Kenya watu wanapokutana huleta hisia ya kuwa kitu kimoja na kuwa kama watu wanaofanana.

Kutokana na utafiti huu, tunapendekeza kwamba wadau kama vile viongozi wanafaa kufanikisha matumizi rasmi ya Kiswahili bila upendeleo wa lugha moja wanapohutubia mikutano ya hadhara. Hali hii itaweza kuleta usawa miongoni mwa wazungumzaji wa lugha mbalimbali katika tarafa ya Kitengela na pia kusaidia kufanikisha harakati za uongozi. Kwa kuwa lugha ni kama sehemu ya utamaduni wa jamii, wadau hao vilevile wachukue jukumu la kuendeleza lugha ya taifa na pia lugha ya asili kwa kuwa kila moja ina jukumu lake muhimu. Hivyo basi tunapendekeza tafiti zaidi kufanywa kuhusu masuala yafuatayo:

1. Utafiti ufanywe kwa kuhusisha wadau wengine kama vile walimu ili kuchunguza mielekeo yao kuhusu lugha ya Kiswahili katika shule za kibinafsi na vilevile za umma katika kaunti ya Kajiado.
2. Utafiti ufanywe kuhusu hali ya lugha asili ya Kimaasai kwa kulinganisha maeneo yaliyo karibu na miji pia mbali na miji.
3. Katiba mpya ya Kenya ya 2010 inatambua Kiswahili na Kiingereza kama lugha rasmi nchini. Hivyo basi utafiti ufanywe ili kulinganisha mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu lugha hizi mbili.

MAREJELEO

- Best, W.J. na J.V Kahn (2010). *Research in Education, New Jersey U.S.A*: Person Prentice.
- Brenzinger, M. (ed.) (1998) 'Endangered Languages in Africa' KöIn: Rüdiger Kö <http://unesco.org/culture/es/files/8283/11195176347> Language _ Vitality _ and _ Endangerment pdf [accessed 4.07.2016]
- Chapurukha, M. Kusimba & Sibel, B. Kusimba. (2003). *East African Archaeology, Foragers, potters, Smiths and Traders*. Philadelphia: University of Pennsylvania Museum of Archaeology and Anthropology.
- Chimera, R. (1998). *Kiswahili, Past, Present and Future Horizons*: Nairobi; Nairobi University Press.
- Chiraghdin, S. na Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili*, OUP, Nairobi.
- Creswell, J.W. (2007). *Educational Research Planning and Evaluation: Qualitative and Quantitative Research* (2 ed) Ohio: Prentice Hall, Inc.
- Edwards, J. R. (1985). *Language, Society and Identity*. New York: Basil Blackwell.
- Ellis, F. (1988). *Peasant Economics : Farm Households and Agrarian Development*. Cambridge University Press.
- Fasold, R. (1984). *The Sociolinguistics of Language*. Massachusetts: Newburyhouse.
- Hardin, G. (1968). *The Tragedy of the Commons*. Science Vol.162-1248-48.
- IribeMwangi, P. na Mukhwana, A. (2011). *Isimu Jamii*; Nairobi; Focus Publishers.
- Okungu, J. (2006). *The Beauty and Shame of Kenya's Constituency Development Fund*, Afroarticles.com.
- Kombo, D. K. & D. Tromp. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi. Paulines Publication Africa.
- Kimani, K. & J. Pickard. (1998). *Recent Trends and Implications of Group Ranch Subdivision and Fragmentation in Kajiado District Kenya*.
- Kratli, S. & Dyer, C. (2009). *Educating Mobile Pastoralist: A strategic review of Literature*. Education Nomads issues paper. London.
- Landweer, M. (2000). "Indicators of Ethno Linguistic Vitality" Notes on Sociolinguistics pg 5-22 [online: <http://www.s.l.org/socialx/ndg/-ig-indicators.html>]

- Lune, H. et al. (2010). *Perspective in Social Research Method and Analysis*. Thousand Oaks: SAGE Publication Inc.
- Lambert, W. (1968). "A study of the Roles of Attitudes and Motivation in Second Language Learning." Fishman J. (mha) *Readings in the Sociology of Language*. The Hague Mouton.
- Mazrui, A. & Mazrui, M. (1995). *Swahili State and Society: The Political Economy of an African Language*, East African Education Publishers, Nairobi.
- Mbaabu, I. (1991). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*. Nairobi: Longman Kenya.
- Mbaabu, I. (1978). *Kiswahili Lugha ya Taifa*. Kenya Literature Bureau.
- Msanjira, P. Y. Kihore & Massamba, D. (2009). *Isimu Jamii Sekondari na Vyuho*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Mohochi, S. (2011). *Mielekeo ya Wasomi wa Kiswahili na Viongozi wa Afrika Mashariki kuhusu Lugha ya Kiswahili*. *Swahili Forum*. 18:24-36.
- Mugenda, M. & Mugenda, G. (2003). *Research Methods Qualitative and Quantitative Approaches Nairobi*: Acts Press.
- Mukhwana, A. (2008). *Language Attitude in Urban Kenya. A Case Study of Nairobi, Kisumu na Mombasa: Tasnifu ya uzamifu (PhD)*, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Mukhwana, A. (2014). Attitude Towards Kiswahili in Urban Kenya: *International Journal of Scientific Research and Innovative Technology* .Vol. 1 No.3;October 2014.
- Mwangi, L. N.(1994). *Optimization of Pastoral Subsistence Strategies under Drought and Marketing Risks.Maasai Model Ranch Study (dissertation)*.Fort Collins: Colorado State University.
- Njoka, T. J. (1979). *Ecological and Socio-cultural Trends of Kaputiei Group Ranches in Kenya*. Ph.D.dissertation, University of California Berkely.
- Ole Katampoi, et al. (1990). *Kajiado District Atlas. Kajiado Kenya:Asal and Programme Kajiado and Ministry of Reclamation and Development of Arid, Semi-Arid areas Westlands*.
- Onyango, J.O.(1990). *Mielekeo ya Wasomi kuhusu Matumizi ya Kiswahili nchini Kenya: Tasnifu ya uzamili*: Chuo Kikuu cha Kenya.
- Owala A. (2014). *Mitazamo kuhusu Kiswahili Miongoni mwa Wazungumzaji wa Kijaluo: Kifani cha Shule za Msingi katika Kaunti ya Migori: Tasnifu ya uzamili*: Chuo Kikuu Nairobi.

- Republic of Kenya (1994). *Kajiado Development Plan 1994-1996*. Office of the Vice-President and Ministry of Planning and National Development. Nairobi.
- Republic of Kenya (1992). *Development of Policy for the Arid and Semi-Arid Lands ASAL*. Nairobi.
- Rutten, M. (1992). *Selling Wealth to buy Poverty: The Process of the Individualization of Land Ownership among the Maasai Pastoralists of Kajiado District, Kenya, 1890-1990*. Fort Lauderdale, FL: Verlag Breitenbach.
- Wanyonyi, E. (2001). *Melekeo ya Walimu wa Kiswahili kuhusu Kiswahili; Hali katika Shule za Upili katika Tarafa ya Emuhaya, Wilayani Vihiga: Tasnifu ya uzamili: Chuo Kikuu Cha Moi*.
- Wendo, N. (2009). 'Language Policy in Kenya: Negotiation with Hegemony' *The Journal of Pan African Studies*, vol.3, no.1. pp 121-138.
- White, J. & S. Meadows (1981). *Evaluation of the Contribution of Group and Individual Ranches in Kajiado District, Kenya*. Ministry of Livestock Development, Nairobi.
- Whitely, Winfred. H. (1969). *Swahili: The Rise of a National Language*. OUP, 1969 Language in Kenya. OUP Nairobi.

VIAMBATANISHO

KIAMBATISHO CHA KWANZA

BARUA YA KUJITAMBULISHA KWA WATAFITIWA

GLADYS NAISEI KAINDI.

S.L.P. 447.

KITENGELA.

12 Januari 2016

KUH: MIELEKEO YA JAMILUGHA YA KIMAASAI KUHUSU KISWAHILI.

Mimi ni mwanafunzi wa shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Ninafanya utafiti kuhusu mada iliyotajwa hapo juu. Naomba unisaidie kujaza hojaji zilizoambatishwa na barua hii, kwa uaminifu. Nakubali ya kwamba majibu yako pamoja na utambulisho wako vitakuwa vya siri mno. Habari nitakazozipokea kutoka kwa hojaji zenyewe zitatumwa tu katika utafiti wangu.

Shukrani kwa ushirikiano wako.

Wako mwaminifu,

GLADYS NAISEI KAINDI

KIAMBATISHO CHA PILI.

HOJAJI KWA VIONGOZI WA KISIASA

Kwa Bi/Bwana _____

Huu ni utafiti unaochunguza mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu Kiswahili katika Tarafa ya Kitengela. Tafadhali yajibu maswali yote kwa kutoa majibu mwafaka, ukizingatia maswali uliyoulizwa. Habari nitakazozipokea kutoka kwa hojaji zitakuwa za siri mno. Ushirikiano wako utakuwa wa manufaa.

1. Jina la Wadi unayoongoza _____

2. Eleza jinsia yako (Tia alama (√))

Mke Mume

3. Tia alama kwenye umri wako.

Chini ya miaka 25

Kati ya miaka 25-30

Kati ya miaka 30-39

Zaidi ya miaka 40

4. Umekuwa kiongozi katika wadi hii kwa muda wa miaka mingapi?

5. Kuna Lokesheni ngapi katika Wadi yako? _____

6. Unaishi katika Lokesheni gani ya Wadi yako? _____

7. Katika Wadi yako kuna Lokesheni zilizo karibu na mji wa Kitengela?

Ndio La

(b) Tafadhali toa maelezo zaidi _____

8 .Katika Wadi unayoongoza, kuna jamiilugha zingine mbali na jamiilugha ya Kimaasai?

Ndiyo La

9. Unaweza kuzungumza lugha zipi?

10. (a) Ungependelea kutumia lugha ipi unapohutubu katika mkutano wa hadhara?

Kiswahili _____ Kiingereza _____ Kimaasai _____

Kuchanganya yote _____

(b)Tafadhali toa sababu ya jibu ulilochagua _____

11. Maoni yako ni yapi kuhusu kauli ya katiba ya Kenya kwamba Kiswahili ni lugha ya

Taifa nchini Kenya ni yapi? _____

12. (a) Kwa maoni yako kuna manufaa ya lugha ya Kiswahili kutumika kama lugha rasmi

nchini Kenya? Ndio La

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako _____

13(a). Kwa maoni yako kuna manufaa ya lugha ya Kimaasai kutumika katika kuwahutubia

wananchi? Ndio La

(b)Tafadhali eleza sababu za jibu lako _____

14.Unaweza kusemaje kuhusu upeo wako wa matumizi ya lugha zifuatazo ?(chagua

mojawapo ya majibu haya : Upeo wa juu,upeo wa kati,upeo wa chini)

(a)Kiswahili _____

(b) Kimaasai _____

(c) Kiingereza _____

15. (a) Ninayaonea fahari mazungumzo rasmi kwa kutumia lugha ya Kimaasai kuliko Kiswahili au Kiingereza. Ndio ____ La ____

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako

16 (a) Kuna manufaa katika kutunza, kukuza na kuendeleza matumizi ya lugha za kienyeji za Wakenya kama vile lugha ya Kimaasai? Ndio ____ La ____.

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako

17(a) .Una ufahamu wowote kuhusu mielekeo ya lugha ya Kiswahili miongoni , mwa wazungumzaji wa lugha ya Kimaasai katika Wadi au eneo unaloongoza?

Ndio ____ La ____.

(b) Tafadhali toa maelezo ya jibu lako.

18. (a) Mwelekeo wako ni upi kuhusu lugha ya Kiswahili ? Chanya ____ Hasi ____.

(b) Tafadhali toa sababu za jibu lako

19 .Maoni yako ni yapi kuhusu mustakabali wa lugha ya Kiswahili Kenya?

20. Kwa maoni yako unafikiri hali ya lugha ya Kimaasai itakuwaje hapo baadaye?_____

Nashukuru sana kwa muda ulionipa .Mchango wako umekuwa muhimu sana katika utafiti huu.

MASWALI YA KUFUATILIA

1.(a)Unapendelea kutumia lugha gani unapohutubia mkutano wa hadhara ?(a) Kiingereza_____

(b) Kiswahili_____ (c) Kimaasai_____ (d)Kuchanganya zote_____

(b) Toa sababu ya jibu lako.

2. Wakazi wengi wa Wadi yako huweza kutumia lugha ya Kiswahili kwa kuuliza au kujibu maswali yanayohusu shughuli za kawaida.(Chagua mojawapo)

(1) Ninakubaliana kabisa (2) Ninakubaliana (3) Sikubaliani kabisa (4) Sikubaliani (5) Sina maoni

3. Mara nyingi watu ambao hawajaelimika katika nchi ya Kenya ndio hutumia lugha ya Kiswahili katika mazungumzo 1 2 3 4 5

(Chagua moja kwa kufuata mfumo wa swali la pili hapo juu)

4. Wafanyikazi wote wa serikali katika nchi ya Kenya wanaowahudumia watu wanapaswa kufahamu lugha ya Kiswahili. 1 2 3 4 5

(Chagua moja kwa kufuata mfumo wa swali la pili hapo juu)

5. (a) Ni lugha ipi unayotumia hasa nyumbani? Kimaasai_____ Kiswahili_____

Kiingereza _____Kuchanganya zote_____

(b) Kwa nini?

6 .Ni manufaa yapi unayoyapata hasa kwa kuwa mwana-jamiilugha ya Kimaasai?

Yapo_____ Hayapo_____ .

7. Tafadhali eleza sababu za jibu lako kwenye swali la 6.

8. Ni manufaa yapi utakayoyapata au kufurahia kama mtu binafsi na mwana-jamiilugha ya

Kimaasai unapotumia lugha yako ya mama ya Kimaasai unayoifahamu vyema na

unayojitambulisha kuwa ni lugha yako?

9. (a) Unaweza kupendelea lugha ya mama (Kimaasai)kutumika katika elimu Kenya ?

Ndio_____ La _____

(b) Unafikiri ni Kwa nini?

10. (a) Ni lugha gani unayoonelea ingekuwa bora zaidi kama mwanao angetumia katika

masomo yake shuleni kwa kuzingatia maisha yake ya baadaye Kenya na dunia kwa ujumla?

Kimaasai _____ Kiswahili_____ Kiingereza. _____

(b) .Tafadhali eleza sababu za jibu lako.

Nashukuru sana kwa muda ulionipa .Mchango wako umekuwa muhimu sana katika utafiti huu

KIAMBATISHO CHA TATU

HOJAJI KWA KIONGOZI WA LOKESHENI

Kwa Bwana /Bi -----

Huu ni utafiti unaochunguza mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu Kiswahili katika Tarafa ya Kitengela. Tafadhali yajibu maswali yote kwa kutoa majibu mwafaka ukizingatia maswali uliyoulizwa. Habari nitakazozipokea kutoka kwa hojaji zitakuwa za siri mno. Ushirikiano wako utakuwa wa manufaa.

1. Jina la Lokesheni unayoongoza. _____

2. Eleza jinsia yako. Mume _____ Mke. _____

3. Tia alama kwenye umri wako;

Chini ya miaka 25 _____

Kati ya miaka 25-30 _____

Kati ya miaka 30 -39 _____

Zaidi ya miaka 40 _____

4. Umeongoza Lokesheni hii kwa muda wa miaka mingapi? _____

5. Kuna Lokesheni ndogo ngapi katika Lokesheni unayoongoza? _____.

6. Unaishi katika Lokesheni ndogo gani? _____.

7. Katika Lokesheni unayoongoza kuna Lokesheni ndogo iliyo karibu na mji wa Kitengela?

(Ndio au La) _____ (Iwapo ipo ni ipi) _____

8. (a) Katika Lokesheni yako kuna jamiilugha zingine mbali na jamiilugha ya Kimaasai?

Ndiyo _____ La _____

(b) Tafadhali toa maelezo zaidi

9. Unaweza kuzungumza lugha zipi? _____, _____, _____,
_____, _____, _____

10. (a) Unapendelea kutumia lugha ipi unapohutubia mkutano wa hadhara?

Kiswahili _____ Kimaasai _____ Kiingereza _____ Kuchanganya zote _____

11. Maoni yako ni yapi kuhusu kauli ya katiba ya Kenya kwamba Kiswahili ni lugha ya Taifa nchini Kenya?

12. (a) Kwa maoni yako kuna manufaa ya Kiswahili kutumika kama lugha rasmi nchini Kenya ?

La _____ Ndio _____

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako.

13. (a) Kwa maoni yako, kuna manufaa ya lugha ya Kimaasai kutumika katika kuhutubia katika mikutano ya hadhara ? Ndio _____ La _____.

(b) Tafadhali toa sababu za maelezo yako.

14. Una sababu zipi zinazokufanya wewe kutumia lugha ya Kimaasai katika mawasiliano ilhali unafahamu kuwa lugha za Kiingereza na Kiswahili ndizo nyenzo mwafaka za mawasiliano?

15. (a) Ni lugha zipi kwa maoni yako, zinazoweza kuimarisha umoja wa makabila mbalimbali nchini Kenya?

(b) Tafadhali toa sababu za maoni yako.

16. (a) Unapendelea kutumia lugha gani hasa kwa mawasiliano unapokuwa kwako nyumbani?_____.

(b) Unafikiri ni kwa nini?

17. Ni manufaa yapi utakayoyapata au kufurahia kama mtu binafsi na mwana-jamilugha ya Kimaasai unapotumia lugha yako ya mama ya Kimaasai unayoifahamu vyema na unayojitambulisha nayo kuwa ni lugha yako.

18. Unaweza kupendelea lugha ya mama (Kimaasai), kutumika katika elimu Kenya?
Ndio____ La_____.

19. Tafadhali toa maelezo ya sababu yako.

20 (a) .Ni lugha gani unayoonelea ingekuwa bora zaidi kama mwanao angetumia katika masomo yake shuleni kwa kuzingatia maisha yake ya baadaye Kenya na duniani kwa jumla?

Kiingereza _____ Kiamaasai _____ Kiswahili _____

Lugha zote tatu _____.

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako

Nashukuru sana kwa muda ulionipa. Mchango wako umekuwa muhimu sana katika utafiti huu.

KIAMBATANISHO CHA NNE

HOJAJI KWA KIONGOZI WA KANISA

Kwa Bi/Bwana---

Huu ni utafiti unaochunguza mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu Kiswahili katika Tarafa ya Kitengela .Tafadhali yajibu maswali yote kwa kutoa majibu mwafaka, ukizingatia maswali uliyoulizwa.Habari nitakazozipata kutoka kwa hojaji zitakuwa za siri mno.Ushirikiano wako utakuwa wa manufaa kwa utafiti huu.

1. Kanisa lako ni la madhehebu gani?_____
2. Eleza jinsia yako. Mke_____ Mume_____
3. Tafadhali eleza kiwango chako cha elimu_____
4. Tia alama kwenye umri wako
 - Chini ya miaka 25
 - Kati ya miaka 25-30
 - Kati ya miaka 30-39
 - Zaidi ya miaka40
5. Umehubiri katika kanisa uliloko kwa muda wa miaka mingapi? _____
6. (a) Kuna washirika kutoka jamiilugha zingine katika kanisa lako mbali na wale wa jamiilugha ya Kimaasai? Ndio La
- (b)Tafadhali toa maelezo zaidi

7. (a) Je, unapendelea kutumia lugha gani unapohubiri kanisani? (a) Kimaasai_____
- (b) Kiswahili _____ (c) Kiingereza _____ (d) Kuchanganya lugha zote tatu_____.

(b) Tafadhali toa sababu za jibu lako

8. (a) Je, wewe hupendelea kutumia Biblia ya lugha gani unapohubiri?

Kiswahili_____Kiingereza_____Kimaasai_____

(b). Tafadhali eleza sababu za jibu lako.

9. (a) Kwa maoni yako, waumini wa kanisa lako hupendelea kuimba nyimbo zilizo katika lugha gani? _____

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako.

10. (a) Kwa maoni yako, kuna manufaa yoyote kwa lugha ya Kiswahili kutumika katika kufundisha au kuhubiri kanisani? Ndio _____ La _____

(b). Tafadhali toa sababu za jibu lako.

11.(a) .Kwa maoni yako, kuna manufaa yoyote kwa lugha ya Kimaasai kutumika katika kufundisha au kuhubiri kanisani? Ndio _____ La _____

(b) Tafadhali eleza maoni yako.

12. Una sababu zipi zinazokufanya wewe kutumia lugha ya Kimaasai katika mawasiliano ilhali unafahamu kuwa lugha za Kiingereza na Kiswahili ndizo nyenzo mwafaka za mawasiliano Kenya?

13 (a).Ni lugha ipi, kwa maoni yako, ungependelea itumiwe na viongozi katika kuhutubia mkutano wa hadhara? _____

(b). Tafadhali eleza sababu za jibu lako

14 (a).Ni lugha zipi, kwa maoni yako, zinaweza kuimarisha umoja wa makabila mbalimbali nchini Kenya?

(b).Tafadhali eleza sababu za maoni yako.

15(a). Kuna manufaa katika kutunza, kukuza, na kuendeleza matumizi ya lugha za kienyeji za Wakenya kama vile lugha ya Kimaasai? (Sema ndio au la)_____

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako.

16(a) Unapendelea kutumia lugha gani hasa unapokuwa kwako nyumbani?

(b) Unafikiri ni kwa nini?

17(a) Ni lugha gani unaonelea ingekuwa bora zaidi kama mwanao angetumia katika masomo yake shuleni kwa kuzingatia maisha yake ya baadaye Kenya na dunia kwa jumla?

Kiswahili _____ Kiingereza _____ Kimaasa _____ Lugha zote tatu _____

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako. _____

18. Maoni yako ni yapi kuhusu hali ya baadaye ya lugha ya Kimaasai?

19. Kwa maoni yako waumini wa kanisa lako wana mielekeo ipi kuhusu lugha ya Kiswahili?

Chanya _____ Hasi _____

Nashukuru sana kwa muda ulionipa .Mchango wako umekuwa muhimu sana katika utafiti huu.

KIAMBATANISHO CHA TANO

Maswali ya kufuatilia

(1) (a) Unapendelea kutumia lugha gani unapohubiri? (a) Kimaasai (b) Kiswahili (c)

Kiingereza

(b) Tafadhali toa sababu za jibu lako

(2) (a) Waumini wa kanisa lako hupendelea matumizi ya lugha gani katika ksoma Biblia, mafundisho na mahubiri? (a) Kimaasai (b) Kiswahili (c) Kiingereza

(b) Tafadhali toa sababu ya jibu lako

(3) (a) Waumini wa kanisa lako huweza kutumia lugha ya Kiswahili kwa kuuliza au kujibu maswali yanayohusu shughuli za kawaida? Ndio_____ La_____

(b) Tafadhali toa sababu ya jibu lako

(4) (a) Unapendelea viongozi wako kutumia lugha gani wanapohutubia mkutano wa hadhara?_____

(b) Tafadhali toa sababu za jibu lako

(5) (a) Kuna manufaa katika kutunza, kukuza na kuendeleza matumizi ya lugha za kienyeji za Wakenya kama vile lugha ya Kimaasai? Ndio_____ La _____

(b) Una sababu gani kuhusu jibu lako?

(6) Una ufahamu wowote kuhusu mielekeo ya lugha ya Kiswahili miongoni mwa wazungumzaji wa Kimaasai katika kanisa lako? Ndio_____ La_____

(7) Mwelekeo wako ni upi kuhusu lugha ya Kiswahili?

(8) (a) Unapendelea kutumia lugha gani ukiwa nyumbani?_____

(b) Kwa nini

(9) (a) Unaweza kupendelea lugha ya mama (Kimaasai), kutumika katika elimu Kenya? Ndio_____ La_____

(b) Tafadhali toa sababu za jibu lako

(10) (a) Ni lugha gani unayoonelea ingekuwa bora zaidi kama mwanao angetumia katika masomo yake shuleni kwa kuzingatia maisha yake ya baadaye Kenya na dunia kwa jumla?

Kiswahili _____ Kimaasai _____ Kiingereza _____

(b) Tafadhali toa sababu za jibu lako

(11) Una maoni gani kuhusu hali ya baadaye ya lugha ya Kimaasai?

Nashukuru sana kwa muda ulionipa. Mchango wako umekuwa muhimu sana katika utafiti huu.

KIAMBATANISHO CHA SITA

HOJAJI KWA WAKAZI KATIKA TARAFI YA KITENGELA

Kwa Bwana/Bi_____

Huu ni utafiti unaochunguza mielekeo ya jamiilugha ya Kimaasai kuhusu Kiswahili katika Tarafa ya Kitengela. Tafadhali yajibu maswali yote kwa kutoa majibu mwafaka, ukizingatia maswali uliyoulizwa. Habari nitakazozipokea kutoka kwa hojaji zitakuwa za siri mno. Ushirikiano wako utakuwa wa manufaa.

1. Jinsia: Kike_____Kiume_____

(Tia alama x kwenye jibu ulilochagua)

2. Umri (Chagua moja kati ya a,b ,c nac)

(a) Kati ya miaka 20 na 25 (b) Kati ya miaka 25 na 30 (c) Kati ya miaka 30 na 40 (d)

Zaidi ya miaka 40

3. Kiwango chako cha elimu

Chini ya kidato cha nne_____

Kidato cha nne_____

Stashahada/Diploma _____

Shahada _____

Mengine (elezea zaidi)

4. Kazi unayoifanya _____

5. (a) Unapendelea kutumia lugha gani unapowasiliana na wenzako kama vile marafiki?

Kiswahili _____Kimaasai _____Kiingereza_____

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako

6. (a) Kwa maoni yako, kuna manufaa yoyote ya Kiswahili kutumika kama lugha rasmi katika mikutano nchini Kenya ? (Sema Ndio au La) _____

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako

7. (a) Kwa maoni yako ungependelea viongozi katika tarafa hii kutumia lugha gani wanapohutubia mikutano ya hadhara? Kiswahili_____ Kimaasai_____ Kiingereza_____

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako

8. (a) Kwa maoni yako kuna manufaa yoyote ya Kimaasai kutumika katika kuhutubua wananchi?(Sema Ndio au La) _____

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako

9. Ukiwa kazini, wewe hutumia lugha gani?

10. Unatumia lugha yako ya kiasili wakati gani?

11. Maoni yako ni yapi kuhusu lugha yako ya Kiasili?

12. (a) Ninayaonea fahari mazungumzo rasmi kwa kutumia lugha ya Kiingereza kuliko Kiswahili au Kimaasai (Sema Ndio au La) _____

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako

13. (a) Ninayaonea fahari mazungumzo ya nyumbani kwa kutumia lugha yangu asilia kuliko lugha Ya Kiswahili (Sema Ndio au La) _____

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako.

14. (a) Kuna manufaa katika kutunza, kukuza na kuendeleza matumizi ya lugha za kienyeji za Wakenya kama vile lugha ya Kimaasai?

Ndio _____ La _____

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako

Chanya _____ Hasi _____

(b). Tafadhali toa sababu za jibu lako

16. Maoni yako ni yapi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili?

17. Maoni yako ni yapi kuhusu hali ya hapo baadaye ya lugha ya Kimaasai?

Maswali ya viwango

Tafadhali piga mviringo (0) katika taarifa uliyopewa hapo chini ukionyesha kwamba;

1. Ninakubaliana kabisa.
2. Ninakubaliana.
3. Sikubaliani kabisa
4. Sikubaliani
5. Sina maoni.

(a) Kiswahili ni lugha inayostahili kutumika katika mawasiliano yetu ya kila siku.

1 2 3 4 5

(b) Lugha ya Kiswahili hutumiwa sana na watu wenye viwango vya chini vya elimu.

1 2 3 4 5

(c) Wafanyikazi wote wa serikali wanaoshughulikia umma wanastahili kufahamu lugha ya

Kiswahili

1 2 3 4

(d) Ni vigumu kuzungumzia shughuli za serikali katika lugha ya Kiswahili

1 2 3 4

(e) Kiswahili ni lugha iliyo na manufaa katika maisha kwa jumla.

1 2 3 4

Nashukuru sana kwa muda ulionipa. Mchango wako umekuwa muhimu sana katika utafiti huu.

KIAMBATANISHO CHA SABA

HOJAJI YA UTAFITI KWA LUGHA YA KIMAASAI

Enetii Ole/Ene_____

Ore ena naa ejurro najurru irrekiei lenkutuk e Kimaasai eimu Kiswahili Kitengela. Aomon tawalu inkikilikuanat pookin aitobiraki, intirrishaki inkikilikuanat nikinkilikuanaki. Ore pookin nilimu naa inainei openy. Ore naboisho ino o nanu enetipat oleng.

1. Enkitok_____ Olee_____

(Tipika × tewueji nitawalua)

2. Ilarin

(Tegelu nabo te a, b, c, aashu c)

(a) Terishata oo larin 20 oo 25 (b) Erishata oo larin 25 oo 30 (c) Erishata oo larin 30 oo 40

(d) Egiroro ilarin 40.

3. Enitabakia tenkisuma

Abori enkilasi enkilasi e onguan te sekontari_____

Enkilasi e onguan te sekontari_____

Empalai e Diploma_____

Empalai e Digrii_____Kulie (Tolimu/Intalala)

4. Esiai niasita_____

5. (a) Kaa kutuk inyoro airoro tenebo iliboitare anaa ilchoreta.

(b) Tolimu enkipirta ewalata ino

6.(a) Amaa too ndamunot inonok ketii tipat e Kiswahili teneirori te nkop e Kenya?

(Tejo ee aashu a-a) _____

(b) Aomon tolimu enkipirta ewalata ino

7. (a) Amaa to ndamunot inonok inyor teneiro ilarikok lemurua ino aa kutuk too ntumoritin? _____

(b) Aomon tolimuenkipirta ewalata ino.

8. (a) Kamaa ketii tipat teneirorieki iltunganak enkutuk e Kimaasai too ntumoritin? (Tejo ee aashu a-a) _____.

(b) Aomon tolimu enkipirta ewalata ino

9. Amaa itii esiai, kaa kutuk iro iyie? _____

10. Kanu oshi iro enkutuk ino?

11. Kaa ijo tenkaraki enkutuk ino?

12 .(a) Keeta tipat tenairo enkutuk oo lashumpa alang Kiswahili o Kimaasai? (Tejo ee ashu a-a)

(b) Aomon tolimu enkipirta ewalata ino

13. (a) Keeta tipat inkirorot e ang tenairo enkutuk ai alang enkut e Kiswahili? (Tejo ee ashu a-a) _____

(b) Aomon tolimu enkipirta ewalata ino

14.(a) Ketii tipat tenerripi, neitubuluni nelu sii dukuya eirori inkutukie ang e Kenya anaa enkutuk e Kimaasai?

Ee _____ A-a _____

(b) Aomon tolimu enkipirta ewalata ino.

15. (a) Kaa ekipirta ino tialo enkutuk e Kiswahili?

(b) Aomon intayu enkipirta ino

16. Amaa tialo enkutuk e Kiswahili, kaa enino?

17. Kaa enino tenkaraki enkutuk e Kimaasai too ngolong'i napuonu?

Inkikilikuanat

Tipika oimosori (o) too mbaa nikinchooki tiabori teine intodolu nchere;

1. Kanyorraa pi.

2. Kanyorraa.

3. Manyorraa pi.

4. Manyorraa.

5 Maata enajo.

(a) Kenare neirori Kiswahili anaake.

1 2 3 4 5

(b) Keiro iltungana liabori oleng te nkisuma enkutuk e Kiswahili

1 2 3 4 5

(c) Kenare naa ore ilaisiayiak pooki le sirkali neyiolo enkutuk e Kiswahili.

1 2 3 4

(d) Kegol teneirori mbaa e sirkali tenkut e Kiswahili.

1 2 3 4

(e) Keeta Kiswahili tipat tiatua enkishui e anaake

1 2 3 4

Ashe oleng te nkata nikinchoo. Ore nitolimuo pooki naa enetipat tialo ena siai.


KIAMBATANISHO CHA NANE

RANCHI ZA MAKUNDI KAUNTI YA KAJIADO KATIKA MWAKA YA 1969



Kutoka kwa: Dr. Marcel Rutten (African Studies Centre – Leiden)

KIAMBATANISHO CHA TISA
ARDHI ZILIZOGAWIWA WATU BINAFSI KATIKA RANCHI ZA MAKUNDI
KITENGELA (AWALI ILIJULIKANA KAMA OLKINOS)



Kutoka kwa: Dr. Marcel Rutten (African Studies Centre – Leiden)